




**Kortini** madai kutumia silaha wizi wa simu

UKURASA 8




UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Mei 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581326

www.ippmedia.com

guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Kibano nyumba za ibada chaja

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WABUNGE WATOA NENO KIKOKOTOO POLISI

KIKOKOTOO cha mafao asilimia 33 kimeendelea kuwa mwiba huku wabunge wakihoji serikali kwa nini kikokotoo hicho hakifanani na kile...

UKURASA WA 4

### CCM YAPENDEKEZA KUREJESHWA KILIMO MTAALA MPYA ELIMU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeitaka serikali kuutumia mtaala mpya wa elimu unaoandaliwa kuzirejesha zilizokuwa shule za sekondari za mchepuo...

## Unafuu maisha wananchi kushuka bei za vyakula

UKURASA 3



Mabasi yakikimbizana barabarani. **PICHA: BEATRICE SHAYO**



# Mbunge ashauri mwendokasi mabasi zaidi ya kilomita 80

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI: REKODI UGENINI INANIPA MATUMAINI UK.24

**KATUNI** UK.6

# Kibano nyumba za ibada chaja

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika mwaka wa fedha 2023/24 imepanga kuandaa mwongozo wa taratibu za kuabudu na ithibati ya taasisi zinazotoa elimu ya dini.

Imesema katika kudhibiti na kupambana na mmomonyoko wa maadili kwenye jumuiya za kidini na zisizo za kidini, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imesitisha shughuli za taasisi ya kidini ya Spirit Word Ministry iliyoko eneo la Stakishari, Ilala jijini Dar es Salaam.

Waziri wa wizara hiyo, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24 huku ikiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.293.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 510.135 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, Sh. bilioni 678.657 ni mishahara na Sh. bilioni 105.027 ni za miradi ya maendeleo.

Kuhusu jumuiya iliyofungiwa usajili, Masauni alisema ni kutokana na kutoa mahubiri na mafundisho yenye mwelekeo wa kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja na kutoa ujumbe wenye kufifisha jitihada za kupambana dhidi ya vitendo hivyo.

Pia alisema mambo mengine watakayofanya ni kuimarisha ufuatiliaji na utendaji wa taasisi za kidini na zisizo za kidini; kufanya ukaguzi na tathmini ya vihatarishi vya kiusalama kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na kutoa mafunzo yatakayochangia kudumisha amani na utulivu.

"Hadi kufikia Mei, mwaka huu, jumuiya za kidini na zisizo za kidini zilizosajiliwa ni 10,108. Taasisi za kidini 672 zilihakikiwa na vyeti vya usajili 672 vilihuishwa. Zoezi litakwenda hadi Mei 31, mwaka huu.

"Taarifa zimekusanywa zinazohusu idadi ya vituo vya kulea watoto na shule zinazotoa mafundisho ya dini kwa watoto wadogo," alisema.

"Lengo ni kutambua idadi ya vituo au shule za bweni zinazotoa mafunzo yenye mwelekeo unaokinzana na maadili ya nchi, ikiwamo vitendo vya mapenzi ya jinsia moja," alisisitiza.

Alisema kazi ya kuboresha vigezo vya usajili inaendelea kwa lengo la kuhakikisha kuwa jumuiya zinazosajiliwa ni zile zenye kuleta tija na zisizokinzana na mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania.

"Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mienendo ya jumuiya zote nakuchukua hatua kali kwa watu au jumuiya zitakazohamasisha vitendo vya ukiukwaji wa maadili," alisema.

**VIPAUMBELE**

Masauni alisema vipaumbele vya wizara kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na kuendelea kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako na operesheni maalum, kuendeleza ushirikishwaji jamii kwenye ulinzi wa umma na kukamilisha miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa.

"Pia kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali; kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa watumishi na askari na kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwamo magari, boti, helikopta, pikipiki pamoja na mitambo na dhana za kisasa.

"Kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani, ili kupunguza matukio ya ajali na kufanya mapitio ya sheria nyingine zinazohusu wizara na kuandaa kanuni; kuboresha huduma za urekebu wa wafungwa na kuimarisha uzalishaji katika mashamba ya magereza kwa ajili ya mahitaji ya chakula cha wafungwa na mahabusu.

"Kuimarisha mashirika yaliyopo chini ya wizara; kuboresha usimamizi wa watumishi na stahiki zao; kutoa mafunzo kwa watumishi raia na askari ndani na nje ya nchi na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu wizara," alisema.

Pia alisema kuimarisha utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti, kupunguza matumizi ya kuni kwa kutumia nishati mbadala kwenye magereza, makambi ya wakimbizi na vyuo vilivyopo chini ya wizara.

"Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo vya polisi yalikuwa 45,455 ikilinganishwa na makosa 43,771 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hili ni ongezeko la makosa 1,684 sawa na asilimia 3.8.

"Ongezeko la makosa haya makubwa linatokana na watu kujichukulia sheria mkononi, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina, migogoro ya ardhi na mirathi, mmomonyoko wa maadili na tamaa ya mapenzi," alisema.

**UKATILI KIJINSIA**

Alisema katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya mashauri 14,184 ya matukio ya ukatili wa kijinsia na watoto yalitolewa taarifa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na matukio 12,642 yaliyotokea kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

"Hii ni ongezeko la matukio 1,542 sawa na asilimia 12.2. Kati ya mashauri hayo 4,120 yalipelekwa mahakamani 2,144 yalishinda na 988 yalishindwa," alisema Masauni.

Alisema mpaka sasa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), vitambulisho vilivyogawiwa vimefikia 10,738,070.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
27.05.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **31.05.2023** hadi 06.06.2023 kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka BANDARI YA DAR ES SALAAM kuelekea MZENGA , gari hizo zenye namba za usajili: **NRB97300/NRB54202 DS00TGGP/NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu** - **27.8**
**Mita Upana** - **5.35**
**Mita Kimo** - **4.70 Mita**

3. Njia itakayotumika: **BARABARA YA MANDELA, BARABARA YA MOROGORO hadi MZENGA** kupitia **MLANDIZI,** gari litasafiri muda wa mchana tu. ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED** Kwa Idhini na Mamlaka tuliyopewa na **CRDB BANK PLC** tunatoa notisi ya **SIKU KUMI NA NNE (14) TU, YA KULIPA DENI UNALODAIWA** kuanzia siku ya tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza **DHAMANA** ulizoweka kwenye mkopo kama ratiba inavyoonyesha.

| S\N | JINA LA MDAIWA\MDHAMINI | DHAMANA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | SPELANDO KASSIAN MGIMWA | PLOT NO 408, BLOCK K, KINYANAMBO B, MAFINGA MJINI, TITLE NO 29281 | 19\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 2. | CLEMENT SAID SANGALE | PLOT NO 53, BLOCK C, MAFINGA MJINI, TITLE 9069 | 20\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 3. | SAMWEL JACOB MASASI | PLOT 477 BLOCK A, MAFINGA MJINI, TITLE NO 30492 | 21\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 4. | HORACE HAMPHREY MVELLA | PLOT NO 508,509,510 &511 BLOCK A, IGOWOLE MJINI, TITLE 31144 | 23\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 5. | BARIKI MULILEGE MINGA | PLOT NO 18, BLOCK B, LUBELE IBANDA KYELA, TITLE NO 31547 | 26\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 6. | BARIKI MULILEGE MINGA | PLOT NO 21, BLOCK D LUBELE IBANDA KYELA TITLE NO 23270 | 27\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 7. | LUCAS JOSEPH NGOMBO | PLOT NO 370, MIKUMI KYELA MJINI | 30\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 8. | GOODLOVE ERASTO SANGA | PLOT NO 582, BLOCK F, IWAMBI, JIJINI MBEYA. | 24\06\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
4. Gharama zote za kubadili hatimiliki ni za mnunuzi
5. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0714939933/0713857349**


## Mbunge ashauri mwendokasi mabasi zaidi ya kilomita 80

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Gairo (CCM), Ahmed Shabiby, ameishauri serikali kuifanya mabadiliko ya mwendokasi wa mabasi ya abiria kutoka kilomita 80 kwa sasa hadi 95.

Amesema mapendekezo yake yanatokana na mfumo wa magari yanayotengenezwa sasa ambayo baadhi yanatumia umeme badala ya mafuta kama ya zamani.

Akichangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/23 bungeni jijini hapo jana, Shabiby alisema: "Kwa nini msiweke utaratibu wa kufuata ratiba mwendokasi kilomita 95 kwa saa? Haya magari ya sasa hivi siyo ya mwendokasi wa kilomita 80 hata ukiangalia sheria mwendokasi wa 80 haiko kisheria.

Mbunge huyo alisema magari ya sasa hivi hayatumii breki bali yanatumia umeme.

"Wekeni mwendokasi 95 fuateni time table (ratiba) gari likitoka Dar es Salaam likafika Chalinze limewahi weka pembeni, piga faini. Linakuja mpaka Morogoro weka pembeni lisiondoke," alisema.

Mbunge huyo alisema kuna kipindi magari yalikamatwa eneo la Same na baadhi ya wabunge wakaanza kupiga kelele wananchi wanateseka.

"Siyo wanateseka polisi wafanye kazi yao bila kufuata watu wa siasa. Gari limewahi ratiba inavyokuonyesha weka pembeni piga faini, hiyo ndio ya kumaliza ajali. Kama tuna polisi kila kona na wanashindwa kuangalia ratiba ambazo wanazo za kila gari, haiwezekani kitu kama hicho," alisema.

Kuhusu kurejesha vidhibiti mwendo, alipendekeza utaratibu utumike wa kufuata ratiba na kwa dereva atakayekiuka atozwe faini. Alisema yeye ni msafirishaji anayefanya kazi hiyo takribani miaka 27 na kwamba kuna vitu vingine serikali haitaki kushirikisha wadau na inapowaita huita wapigadebe na si wahusika.

"Mkiita wadau unaita mpigadebe wale wadau wahusika kabisa hamuwaiti kuwapa ushauri toka enzi ya Mwalimu Julius Nyerere kaja Rais Ali Hassan Mwinyi, kaja Benjamini Mkapa, mpaka leo.

"Ukienda LATRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini) kuchukua leseni ya usafirishaji kama unatoka Dar es Salaam kuja Dodoma unapewa kitu kinaitwa 'timetable' (ratiba) kwamba gari litatoka Dar es Salaam saa ngapi na kufika Chalinze saa ngapi? Litafika Morogoro saa ngapi? Na kufika Gairo saa ngapi? Na Dodoma saa ngapi? Huwekwa kulingana na mwendo ambao basi linatembea," alisema.

Mbunge huyo alisema baadaye wakaleta kidhibiti mwendo ambacho kilifanya kazi kikafeli kwa sababu madereva walikuwa wanakichezea kwa kuweka swichi na vikawa havina kazi yoyote.

"Sasa hivi mmeleta VTS ambayo nayo kuna kipindi inafanya vizuri na kipindi inachezewa. Sasa nimekusikia Mheshimiwa Waziri mnarudisha 'speed gavanor' ambayo ilifeli mwanzoni. Msifanye mchezo nani atanunua kila siku spidi gavana, mtu una magari 60 ukanunue spidi gavana Sh. milioni 1.8 kwa magari 60 na ilishafeli na unajua kabisa dereva ataichezea.

**KIDOLE TRAFIKI**

Mbunge wa Viti Maalum, Angelina Malembeka, alisema kuna baadhi ya maeneo trafiki wanawapa kero akimshika mmoja mwenye spidi ya 90 hata yakipita magari 20, wote wataonyeshwa king'amuzi cha spidi 90 tu.

"Kama hivyo ving'amuzi ni vibovu vikatengenezwe au vinunuliwe vipya, lingine wana mchezo wa kujificha hawa utaona ghafla kakurupuka kwenye mihogo, wewe ni bwana shamba kwenye mihogo umefuata nini?

"Kaa barabarani tukuone kama kuna tatizo tusimame tukwambie. Kuna mwingine anamfuata trafiki amuulize hivi kutoka Gairo mpaka Manyoni ni kilometa ngapi, lakini yeye yuko kwenye mihogo.

Pia alisema baadhi ya trafiki wanaweza kusimamisha mabasi mengi halafu wanakaa ili dereva au utingo amfuate na kusema hiyo imekuwa ikiwatia hasira madereva na matokeo yake huendesha kwa mwendo kasi na kusababisha ajali mbele.

HABARI KITAIFA

# Unafuu bei ya vyakula ikishuka

Na Waandishi Wetu



BEI za vyakula katika mikoa mbalimbali nchini zimeanza kushuka na kuleta unafuu kwa wananchi ambao wameiomba serikali kushusha pia ya sukari ambayo inazalishwa nchini.

Ufuatiliaji uliofanywa na Nipashe kwenye mikoa mbalimbali, umebaini kuwa vyakula vilivyoshuka bei ni mchele, mafuta, unga wa ngano na mahindi kwa wiki tatu sasa.

Hata hivyo, wafanyabiashara na wananchi wameonesha hofu ya bidhaa hizo kupanda tena kutokana na wimbi la wanunuzi kutoka nje ya nchi kufuata kwenye mashamba.

Walitaja sababu za kushuka kwa nafaka hizo kuwa ni msimu wa mavuno na bei ya mafuta ya petroli na dizeli kulikochangia gharama za usafirishaji kupungua.

**DAR ES SALAAM**

Mfanyabiashara wa mchele wa jumla katika soko la Temeke, Dickson James, alisema kwa sasa wanauza mchele kuanzia Sh.1,600 jambo ambalo wiki tatu zilizopita halikuwapo.

"Mchele tuliokuwa tunauza bei ya jumla Sh. 3,500 sasa hivi tunauza 2,800 kwa sababu tunauziwa na wakulima Sh. 2,200 kutoka Sh. 2,800 hapo awali. Ule tuliokuwa tunauza Sh. 2,900 sasa hivi tunauza Sh. 2,200 kwa sababu tulikuwa tunanunua Sh. 2,600 na sasa wakulima wanatuuzia Sh. 1,800," alifafanua Dickson.

Mfanyabiashara wa nafaka hiyo kutoka soko la Ilala, Rajab Salehe, alisema hofu yao ni wafanyabiashara kutoka nchi jirani ikiwamo Kenya kwenda mashambani kununua kwa bei ya juu.

"Tayari nasikia Kilombero Wakenya na Wakongo wameshaingia, wale jamaa huwa wananunua hata heka nzima tena kwa bei ya juu, wanachangia kuwatia wakulima tamaa na kutupandishia bei hata sisi wazawa, serikali inapaswa iweke utaratibu wa kutulinda sisi," alisema.

Mmiliki wa mashine ya kusaga na kuuza unga wa mahindi Tabata, Jasmin Hussein, alisema walishusha mahindi ya makande kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 8,000 kwa mfuko wa kilo tano, huku mfuko wa kilo 10 wakiuza Sh. 16,000 kutoka 17,000 na kilo 25 umeshuka Sh. 39,000 kutoka 42,000.

Mfanyabiashara wa mafuta ya kula, Mohammed Musa, alisema kwa sasa wanauza katoni yenye galoni nne ya mafuta ya alizeti ya lita tano Sh. 95,000 kutoka Sh. 108,000 ya hapo awali, huku mafuta ya Korie ya lita 20 wakiuza Sh. 70,000 kutoka Sh. 75,000 hali iliyosababisha kuuzwa Sh. 3,500 kutoka 4,500 kwa lita moja kwa bei ya rejareja.

Kwa mujibu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara bei za juu za jumla za mazao makuu ya chakula nchini kwa kilo 100 hadi kufikia Mei 12, mwaka huu ni mahindi kwa Sh. 120,000 kutoka Sh. 103,000 mwezi uliopita.

Bei ya mchele ni Sh. 300,000 sawa na mwezi uliopita ambayo imeshuka ukilinganisha na Machi 31 iliyokuwa inauzwa Sh. 320,000 wakati maharagwe yakishuka bei kufikia Sh. 270,000 kutoka Sh. 280,000 Aprili.

**KAGERA**

Mfanyabiashara wa nafaka soko kuu la Bukoba, Lucy Batiromayo, alisema: "Mchele safi uliokuwa ukiuzwa kwa Sh. 4,000 kwa sasa umeshuka mpaka Sh. 3,000 hadi Sh. 3,500 kwa kilo moja huku mchele wa kawaida kwa sasa unauzwa kwa Sh. 2,200 kutoka Sh.3,000."

**MOSHI**

Katika Soko la Mbuyuni na la Kati, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, mchele kilo 25 umeshuka kutoka Sh. 67,000 hadi 61,000 na kilo 50 imepungua kutoka Sh. 140,000 hadi Sh. 132,000.

**MANYARA**

Ally Hamis wa Soko la Babati, alisema mchele kutoka Mbeya, kwa sasa unauzwa Sh. 3,000 kwa kilo moja na mchele wa kawaida wa Magugu unauzwa Sh. 2,800 kwa kilo.

**TANGA**

Katika masoko ya Mgandini na Mlango wa Chuma, mchele umeshuka kutoka Sh. 3,000 hadi Sh. 2,600 kwa kilo moja ya mchele wa Mbeya na wa kawaida unauzwa kwa Sh. 2,400 hadi Sh. 2,200 kwa kilo.

**ARUSHA**

Jijini Arusha kilo moja ya mahindi inauzwa Sh. 1,150 wakati gunia la kilo 100 ni Sh. 120,000.

**MWANZA**

Mchele uliouzwa Sh. 3,000 hadi 3,200 sasa ni Sh. 2,700 hadi 2,800.

Mafuta ya kula yameshuka kutoka Sh. 1,800 hadi Sh.1,500 kwa chupa ya mililita 350.

**SIMIYU**

Mkuu wa Division ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Robert Urasa, alisema alizeti debe moja linauzwa Sh. 4,000, mahindi debe ni kati ya Sh. 14,000 na Sh.16,000, mpunga debe ni kati ya Sh.10,000 na Sh.11,000.

**SHINYANGA**

Mchele unaouzwa kwenye mashine kilo moja ni Sh. 2,400 kutoka Sh. 2,800 mpaka 2,900 huku debe lenye kilo 20 likiuzwa kwa Sh.12,000 hadi 13,000 kutoka bei ya awali ambayo ilikuwa ni Sh. 25,000.

**MOROGORO**

Mmoja wa wamiliki wa duka katika Kata ya Kihonda Magorofani, Zahera John, alisema mchele aliokuwa akiuza kilo 3,200 sasa anauza 2,600, unga kutoka Sh. 1,800 kwa sasa anauza 1,500 na maharage alikuwa akiuza 3,400 sasa Sh. 2,900.

**DODOMA**

Unga wa mahindi (sembe) umeshuka kutoka Sh. 2,800 hadi Sh. 2,000, maharagwe yameshuka hadi Sh. 3,200 kutoka Sh. 4,000 na mchele ni Sh. 2,000 kwa kilo kutoka 3,000 hadi 3,500.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR), Mary Mosha, Anjela Mhando (MOSHI), Jaliwason Jasson (MANYARA), Hamida Kamchalla (TANGA) na Tumaini Mafie (ARUSHA), Neema Emmanuel, (MWANZA), Alex Sayi (SIMIYU), Mohab Dominick (KAHAMA), Titus Mwombeki, (KAGERA), Paul Mabeja (DODOMA) na Ashton Balaigwa (MOROGORO)**


## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

ILEMELA MUNICIPAL COUNCIL
MWANZA

**30/05/2023**

## TANGAZO LA ZABUNI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia wananchi wenye sifa na wafanyabiashara wote, zabuni kwa ajili ya kuwapata wapangaji katika majengo mbalimbali ya Halmashauri yaliyopo stendi ya mabasi na maegesho ya Malori -Nyamhongolo .Taasisi, Wananchi/Kampuni/Kikundi/Ushirika na wafanya biashara wote wenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu.

| NA | NAMBA YA ZABUNI | AINA YA ZABUNI. | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | A. UPANGISHAJI | | | |
| 1. | LGA/159/2023/2024/NC/08 – I JENGO LA ABIRIA | ENEO LA BIASHARA | AINA YA BIASHARA | IDADI YA VYUMBA | KODI KWA MWEZI(TSH) @ |
| | | A:ENEO LA CHINI | I:BENKI | 2 | 4,345,200.00 |
| | | | II:SUPERMARKET | 2 | 3,555,000.00 |
| | | | III:VYUMBA VYA KUKATIA TIKETI | 16 | 155,000.00 |
| | | | IV:MIGHAHAWA | 3 | 561,600.00 |
| | | | V:MADUKA MAKUBWA | 3 | 595,200.00 |
| | | B:GHOROFA YA KWANZA | I:MADUKA MAKUBWA | 7 | 469,800.00 |
| | | | II:VYUMBA VYA KUKATIA TIKETI | 30 | 155,000.00 |
| 2. | LGA/159/2023/2024/NC/08 – II JENGO LA BIASHARA | A:ENEO LA CHINI | I:BENKI | 2 | 2,730,000.00 |
| | | | II:SUPERMARKET | 1 | 2,233,200.00 |
| | | | III:MADUKA MAKUBWA | 2 | 752,400.00 |
| | | B:GHOROFA YA KWANZA | I:MADUKA/OFISI | 10 | 601,800.00 |
| | | C:GHOROFA YA PILI | I:MADUKA/OFISI | 10 | 451,200.00 |
| | | D:GHOROFA YA TATU | I:MADUKA/OFISI | 10 | 300,600.00 |
| 3. | LGA/159/2023/2024/NC/08 – III JENGO LA HOSTEL | A:ENEO LA CHINI-MBELE | I:MADUKA | 5 | 219,000.00 |
| | | | II:MGHAHAWA | 1 | 193,200.00 |
| | | | III: VYUMBA VYA ATM | 3 | 152,400.00 |
| 4. | LGA/159/2023/2024/NC/08 – IV ENEO LA MAEGESHO LA MABASI | A:MAEGESHO YA MABASI | I:MADUKA | 72 | 153,000.00 |
| 5. | LGA/159/2023/2024/NC/08 – V MAEGESHO YA MALORI | A:MAEGESHO YA MALORI | I:MAGHALA | 4 | 1,525,800.00 |
| | | | II: GEREJI | 1 | 932,400.00 |

**MAELEZO KWA WAOMBAJI:**

1. Muombaji lazima awe na leseni hai kwa biashara husika anayokusidia kuitekeleza, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney).
2. Dhamana kwa muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration).
3. Ada ya maombi ya zabuni yatalipiwa kulingana na aina ya zabuni kama ifuatavyo;-
   i. Upangishaji wa eneo la Mabenki,Supermarket na Maghala-TZS 100,000.00
   ii. Upangishaji wa Vyumba vya kukatia tiketi, Mighahawa, Maduka, karakana na Vyumba vya ATM - TZS 50,000.00

   **Fedha hizi hazitarudishwa.** Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo kwa njia ya kielectroniki hayatakubaliwa.Maombi yote ya ambatishwe na picha mbili za passpoti size, za hivi karibuni. Muombaji anaruhusiwa kuomba zabuni zaidi ya moja na kila zabuni ni lazima alipe ada ya maombi ya zabuni husika.
4. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba. Maombi yote yatumwe kwa:-**KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 - MWANZA.**
5. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri, asiwe na historia ya kusababisha migogoro na wala asiombe kwa nia ya kumpangishia mtu mwingine. Iwapo itabainika na kuthibitika atanyang'anywa chumba hicho mara moja na dhamana yake haitarejeshwa.
6. Mwombaji awe na uwezo wa kulipa kodi ya chumba au eneo ndani ya siku saba baada ya kupewa barua ya tuzo,endapo akishindwa kulipa ndani ya siku kumi na nne(14) Halmashauri italazimika kupangisha mpangaji mwingine.
7. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili, endapo maelezo ya halisi na nakala yatatofautiana maelezo yaliyopo kwenye nyaraka halisi ndio yatatumika kwenye tathmini.
8. **Mwisho wa kupokea maombi ni 13/06/2023 saa 6.00 mchana. Maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 mchana hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**
9. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.
10. Waombaji walio ndani ya pango watapewa kipaumbele.

**ENG MODEST J. APOLINARY**
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

ILEMELA MUNICIPAL COUNCIL MWANZA

30/05/2023

## TANGAZO LA ZABUNI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia wananchi wenye sifa na wafanyabiashara wote, zabuni kwa ajili ya kuwapata wapangaji wa majengo mbalimbali ya Halmashauri. Wananchi/Kampuni/Kikundi/Ushirika na wafanyabiashara wote wenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu.

| NA | NAMBA YA ZABUNI | AINA YA ZABUNI. | | |
|---|---|---|---|---|
| | A. UKODISHAJI | | | |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01 - I | **SOKO LA BUZURUGA** | | **KODI @ MWEZI (TZS)** |
| | | i.VYUMBA VYA MBELE | 130 | 180,000.00 |
| | | ii.VYUMBA VYA NDANI | 77 | 80,000.00 |
| | | iii.PARTITION | 6 | 50,000.00 |
| | | iv.MEZA SOKONI | 124 | 9,000.00 |
| | | v. MABANDA YA MACHINGA | 224 | 10,000.00 |
| | | vi.MIGAHAWA | 12 | 10,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01-II | **SOKO LA KITANGIRI** | | **KODI @ MWEZI(TZS)** |
| | | i.VYUMBA VYA MBELE | 44 | 50,000.00 |
| | | ii.VYUMBA VYA NDANI | 16 | 40,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01 - III | **SOKO LA NYAMANORO** | | **KODI @ MWEZI (TZS)** |
| | | i.VYUMBA VYA MBELE | 30 | 50,000.00 |
| | | ii.VYUMBA VYA NDANI | 47 | 40,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01-IV | **SOKO LA MWALONI** | | **KODI @ MWEZI (TZS)** |
| | | i.MEZA ZA MATUNDA | 102 | 50,000.00 |
| | | ii. MEZA ZA NAFAKA | 5 | 50,000.00 |
| | | iii. SAMAKI WA CHUMVI | 3 | 50,000.00 |
| | | iv.SAMAKI WAKAVU | 1 | 50,000.00 |
| | | v. SAMAKI WABICHI | 1 | 50,000.00 |
| | | vi. OFISI | 9 | 30,000.00 |
| | | vii. MIGAHAWA | 20 | 20,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01- V | **SOKO LA NYAKATO** | | **KODI @ MWEZI (TZS)** |
| | | i. VYUMBA VYA MBELE | 50 | 20,000.00 |
| | | ii. VIZIMBA VYA MBAO | 75 | 10,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01-VI. | **SOKO LA NYASAKA CENTRE** | | **KODI @ MWEZI(TZS)** |
| | | i. MADUKA | 298 | 40,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01-VII | **SOKO LA SABASABA** | | **KODI @ MWEZI** |
| | | i. MABANDA YA MAMA LISHE | 86 | 20,000.00 |
| | | ii. MEZA ZA LEVMP | 84 | 10,000.00 |
| | | iii.MEZA ZA KAWAIDA | 212 | 5,000.00 |
| | | iv. MEZA ZA SAMAKI | 36 | 10,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/09-VIII. | **SOKO LA MSUKA** | | **KODI @ MWEZI(TZS)** |
| | | i.VYUMBA VYA MBELE | 70 | 60,000.00 |
| | | ii.VYUBA VYA NDANI | 62 | 40,000.00 |
| | | iii.MEZA | 212 | 9,000.00 |
| | LGA/159/2023/2024/NC/01– IX | **SOKO LA PASIANSI** | | **KODI @ MWEZI (TZS)** |
| | | i. VYUMBA VYA MBELE | 35 | 60,000.00 |
| | | iv. VYUMBA VYA NDANI | 35 | 40,000.00 |
| | | v. MEZA | 350 | 9,000.00 |

**MAELEZO KWA WAOMBAJI:**

1. Muombaji lazima awe na leseni hai kwa biashara husika anayokusidia kuitekeleza, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney).
2. Dhamana kwa muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration).
3. Maombi ya zabuni yatalipiwa kulingana na aina ya zabuni kama ifuatavyo;-
   i. Upangishaji wa Maduka,Ghala na Meza Mwaloni TZS 20,000.00
   ii. Upangishaji wa migahawa, Vizimba na Ofisi TZS 10,000.00
   iii. Upangishaji wa Meza sokoni TZS 5,000.00

**Fedha hizi hazitarudishwa.** Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo kwa njia ya kielectroniki hayatakubaliwa.Maombi yote ya ambatanishwe na picha mbili za passpoti size, za hivi karibuni. **Muombaji anaruhusiwa kuomba zabuni zaidi ya moja na kila zabuni ni lazima alipe ada ya maombi ya zabuni husika.**

4. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba. Maombi yote yatumwe kwa:-**KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 - MWANZA.**
5. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri, asiwe na historia ya kusababisha migogoro na wala asiombe kwa nia ya kumpangishia mtu mwingine chumba, meza,ofisi,migahawa na/au ghala.Iwapo itabainika na kuthibitika atanyang'anywa chumba hicho mara moja na dhamana yake haitarejeshwa.
6. Mwombaji awe na uwezo wa kulipa kodi ya pango ya miezi mitatu(3) ndani ya siku saba baada ya kupewa barua ya tuzo,endapo akishindwa kulipa ndani ya siku kumi na nne(14) Halmashauri italazimika kumuondoa kwa nguvu na kupangisha mpangaji mwingine.
7. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili, endapo maelezo ya halisi na nakala yatatofautiana maelezo yaliyopo kwenye nyaraka halisi ndio yatatumika kwenye tathmini.
8. **Mwisho wa kupokea maombi ni 13/06/2023 saa 6.00 mchana, maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**
9. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.

**MODEST J. APOLINARY.**
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**


# Wabunge watoa neno kikokotoo polisi

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

KIKOKOTOO cha mafao asilimia 33 kimeendelea kuwa mwiba huku wabunge wakihoji serikali kwa nini kikokotoo hicho hakifanani na kile kinachotumika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Usalama wa Taifa.

Wamesema kutokana na fedha za mafao wanazozipata askari na maofisa wa polisi kuwa kidogo, wengi wao wanakufa muda mfupi baada ya kustaafu.

Wakichangia mjadala wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, baadhi ya wabunge walitaka wizara hiyo ijipange kwenye hilo kwa kujali maslahi ya wastaafu wa jeshi hilo.

Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby, alisema: "Kwenye Jeshi la Polisi, wastaafu wanapata tabau. Tunawaona, hata pale Gairo na sehemu zingine. Kikokotoo wanachokitumia cha mafao ni kile cha watumishi wa umma. Kwa nini wasitumie kikokotoo kama wanachotumia JWTZ na Usalama wa Taifa?

"Leo askari anamaliza kazi yake amefanya kazi miaka 30 anakuwa maskini wa kutupwa. Anakufa muda mfupi, hiyo lazima tufanye haki. Wako ambao wanadai mpaka Sh. milioni 100. kwenye wizara mnazidi kuongeza mzigo."

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, katika taarifa yake, alisema licha ya kwamba polisi wanapewa kama watumishi wengine na si kama watumishi wa JWTZ, lakini pia mafao yao na michango wanacheleweshewa na wakistaafu wanapofuatilia mafao yao, wanaambiwa hawawezi kupewa mafao mpaka watoe riba.

"Wakati wajibu wao ni serikali, wengine askari hawa wanafariki dunia hawajapewa mafao yao," alisema.

Mbunge Shabiby alipokea taarifa hiyo na kuendelea na mchango wake kuwa wakati mwingine wanasema askari hao wanakula rushwa na kwamba hata yeye angekuwa polisi angekula.

"Kwa style (hali) hii ndio ukweli lazima mafao yao wayapate, unajua kuna vitu vingi sana vinachangia tu na tunachukia lakini tunaangalia kuanzia mishahara yao? Tunaangalia kuanzia maslahi yao?" alihoji.

Mbunge wa Msalala, Kassim Iddi, alimweleza Masauni kwamba ataandika kitabu chenye historia nzuri kama atafanya mabadiliko na mapinduzi kuboresha Jeshi la Polisi.

"Jeshi la Polisi kwa sasa ukienda kwenye mawanda ya ajira utaona kabisa limepewa kipaumbele cha mwisho katika kuomba au kutafuta ajira. Ukilinganisha na hapo mwanzoni, lilikuwa na heshima kubwa.

"Leo hii kuna baadhi ya maofisa wakiwamo IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) na wengine wanafanya kazi nzuri sana. Kadri siku zinavyokwenda kumekuwa na sintofahamu ndani ya Jeshi la Polisi. Nidhamu weledi rushwa na mambo mengine yote yanasababishwa na maslahi ya askari wetu ni mabaya mno," alisema.

Mbunge huyo alisema askari ambao wanalinda mali na kutoa maisha yao, anafanya kazi miaka 60 anapostaafu anaondoka na Sh. milioni 18.

Mbunge huyo alisema Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu lakini Msalala wana OCD lakini hana gari akienda kukagua tukio anakwenda na bodaboda akishuka amejaa vumbi hata aeleweki.

"Nikuombe kwa uchungu mkubwa hasa sisi tunaotoka kwenye mazingira ya migodi. Cha kusangaza hawa hawa wanalinda mali na migodi mikubwa. Hivi Mheshimiwa Waziri unashindwa kufanya vikao hata na hawa wawekezaji wakubwa kwenye maeneo yetu kuwaomba angalau wachangie mahali kwa sakari wetu wanaolinda mali zao. Boresha maslahi," alisema.

# CCM yapendekeza kurejeshwa kilimo mtaala mpya wa elimu

**Na Nebart Msokwa,**
MUFINDI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeitaka serikali kuutumia mtaala mpya wa elimu unaoandaliwa kuzirejesha zilizokuwa shule za sekondari za mchepuo wa kilimo ili zitumike kuwaandaa vijana kuwa wataalamu wa kilimo na kuwajengea uwezo wa kujiajiri kupitia sekta hiyo.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, aliyasema hayo juzi alipotembelea Shule ya Sekondari Malangali iliyopo katika Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa ambayo ni miongoni mwa shule za awali zilizokuwa za mchepuo wa kilimo.

Alisema kilimo ni moja ya sekta muhimu ambazo zinatakiwa kuwekewa mkazo hasa kwa kuwajengea uwezo vijana kuipenda kutokana na kuajiri idadi kubwa ya watu ikilinganishwa na sekta zingine.

Alisema vijana wakijifunza vizuri kilimo, ufugaji na shughuli zingine za mikono watakuwa na tija zaidi kwa taifa kuliko ilivyo sasa wanaandaliwa kuajiriwa jambo linalosababisha wengi wao kukosa ajira.

"Vijana wetu wakifundishwa vizuri kilimo, ufugaji na kazi zingine za mikono, watakuwa na tija zaidi kwa taifa kuliko ilivyo sasa, mtaala wa sasa unawaandaa vijana wetu kuajiriwa na ndiyo maana wanafika mpaka chuo kikuu, lakini hawawezi hata kutengeneza stuli," alisema Chongolo na kuongeza.

"Tunataka vijana wakijifunza kompyuta basi wafundishwe mifumo yote waijuwe, wakijifunza ufugaji waelewe vizuri ili wakafunge na kufundisha wengine na wale watakaojifunza kilimo wakawe wataalamu kweli," aliongeza. Alisema shule hizo zikirejeshwa, wanafunzi watakuwa wanasoma masomo ya kawaida, lakini mkazo mkubwa utakuwa kwenye kilimo kama ilivyokuwa zamani.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema, aliwataka wazazi na walezi wilayani Mufindi kuwapeleka watoto wao shuleni hasa wa kike ili wapate haki yao ya msingi ya kupata elimu badala ya kuwaozesha kama ambavyo imekuwa ikitokea kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Alisema kwa sasa nchi ina mifano mingi ya wanawake waliofanikiwa na kulisaidia taifa akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni rais pekee mwanamke katika ukanda wa Afrika Mashariki na hivyo akawataka wazazi kutowapuuza.

Vile vile, aliwataka wazazi na walezi kufuatilia vizuri mienendo ya watoto wao wanapokuwa shuleni na wanapokuwa mitaani ili wasijiingize kwenye makundi mabaya ambayo yanaweza kuharibu maadili yao na wakashindwa kufikia malengo yao.

# TANGAZO

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

30/05/2023

## TANGAZO LA ZABUNI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia wananchi wenye sifa na wafanyabiashara wote, zabuni kwa ajili ya kuwapata wapangaji wa jengo la Hosteli vyumba 100 stendi ya mabasi na maegesho ya Malori -Nyamhongolo. Taasisi, Wananchi/ Kampuni/Kikundi/Ushirika na wafanyabiashara wote wenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu.

| NA | NAMBA YA ZABUNI | AINA YA ZABUNI. |
|---|---|---|
| | | |
| | UPANGISHAJI WA VYUMBA 100 JENGO LA HOSTEL | |
| 1 | LGA/159/2022/23/NC/08 - XIV | Upangishaji wa utoaji wa huduma ya malazi katika Jengo la Hostel,Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Malori Nyamhongolo |

### MAELEZO KWA WAOMBAJI:

**A: - VYUMBA 100 VYA HOSTEL**

1. Muombaji lazima awe na leseni hai ya kuendesha biashara ya Guest House au Hotel au Hostel.

2. Muombaji aonyeshe utambulisho wa mlipakodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, ambatanishe Tax Clearance, na Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney inahusika kwa Kampuni tu).

3. Muombaji ataweka samani (Furniture) zake mwenyewe, kwa Mwongozo wa Halmashauri

4. Dhamana kwa Muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration).

5.Maombi ya zabuni yatalipiwa Tshs 100,000.00 Fedha hizi hazitarudishwa. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Maombi yote yaambatishwe na picha mbili za passpoti size, za hivikaribuni.

6. Maombi yote ya fungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba. Maombi yote yatumwe kwa:-**KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 - MWANZA.**

7. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili, endapo maelezo ya halisi na nakala yatatofautiana maelezo yaliyopo kwenye nyaraka halisi ndio yatatumika kwenye tathmini.

8. **Mwisho wakupokea maombi ni 13/06/2023 saa 6.00 mchana. Maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 mchana hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**

9. Dhamana kwa Muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration).

10. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.

**MHANDISI MODEST J. APOLINARY**
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

30/05/2023

## TANGAZO LA ZABUNI

**USAFISHAJI, UKUSANYAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA NYUMBA ZA MAKAZI NA MAENEO YA BIASHARA KWENDA VITUO VYA KUKUSANYIA TAKA NA ENEO LA KUTUPIA TAKA KWENYE HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA KANDA A-C NAMBA I-XVII.**

**KANDA A NI KIRUMBA,KITANGIRI,NYAMANORO,BUZURUGA,MECCO,PASIANS NA NYASAKA.**
**KANDA B NI BUSWELU,NYAKATO,KISEKE,KAWEKAMO NA IBUNGILO**
**KANDA C NI ILEMELA, NYAMHONGOLO,SANGABUYE,BUGOGWA,KAYENZE,KAHAMA NA SHIBULA.**
**ZABUNI Na. LGA/159/2023/2024/NC/ 03**

1. Mwaliko huu wa Zabuni unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa Mwaka 2023/2024 wa fedha unaoonekana.
2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia Wananchi/Kampuni/Kikundi/Ushirika au yeyote mwenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu, kwa ajili ya **USAFISHAJI, UKUSANYAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA NYUMBA ZA MAKAZI NA MAENEO YA BIASHARA KWENDA VITUO VYA KUKUSANYIA TAKA NA ENEO LA KUTUPIA TAKA KWENYE HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA KANDA A-C NAMBA I-XVII.**
3. **WAOMBAJI WA KATA ZA KITANGIRI, NYAMANORO, IBUNGILO, PASIANS, KAWEKAMO, BUZURUGA, MECCO,ILEMELA NA NYAKATO WATASAFIRISHA TAKA KUTOKA KWENYE MAKAZI (HOUSEHOLDS)/SEHEMU ZA KUZALISHIA TAKA KWENDA DAMPO BUHONGWA.**
4. **WAOMBAJI WA KATA ZA NYAMHONGOLO, KISEKE, BUSWELU, KIRUMBA, BUGOGWA, SHIBULA NA NYASAKA WATASAFIRISHA TAKA KUTOKA KWENYE NYUMBA ZA MAKAZI/SEHEMU ZA KUZALISHIA TAKKWENDA VITUO VYA KUKUSANYIA TAKA.**

| KATA/KANDA | ENEO LINALOOMBWA /MTAA | ZABUNI NAMBA | KANDA |
|---|---|---|---|
| KIRUMBA | Magomeni | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | A |
| | Ngara | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Kirumbakati | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Mlimani A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Kiyungi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Mlimani B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Kigoto | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Kabuhoro A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/I | |
| | Kabuhoro B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| KITANGIRI | Kileleni | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | A |
| | Jiwekuu | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Kitangirikati | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Mwinuko | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Kitangiri A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Kitangiri B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Medical | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| | Mihama | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/II | |
| NYAMANORO | Nenetwa | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | A |
| | Mkudi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| | NyamanoroMashariki | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| | Kilimahewa A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| | Kilimahewa B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| | Mnyampara | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| | Nyamanoro | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IV | |
| IBUNGILO | Kiloleli A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | B |
| | Kiloleli B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| | Nyamanoro C | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| | Nyamanoro D | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| | NyamanoroKaskazini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| | Ibungilo A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| | Ibungilo B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/V | |
| KAWEKAMO | Nyasaka A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | B |
| | Nyasaka B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | |
| | Nyasaka C | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | |
| | Msumbiji | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | |
| | PasiansiMashariki A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | |
| | PasiansiMashariki B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VI | |
| PASIANSI | Pasiansijuu | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | A |
| | Pasiansichini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | |
| | PasiansiMagharibi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | |
| | Bwirumchangani | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | |
| | Bwiru Press | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | |
| | BwiruBima | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VII | |
| ILEMELA | Butuja | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | C |
| | Bukengwa | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Kahasa | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Nyagungulu | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Ilemela | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Balyehele | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Mwambani | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Madukuru | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | Saba saba | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| | LumalaMashariki | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/VIII | |
| MECCO | MeccoMashariki | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IX | A |
| | MeccoKaskazini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IX | |
| | MeccoKusini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IX | |
| | Nundu | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IX | |
| | Gedelikivukoni | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/IX | |
| NYAKATO | Ihangilo | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | B |
| | Kangaye A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | Kangaye B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | Gedeli | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | National Magharibi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | National Mashariki | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | Majengomapya | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | National | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| BUZURUGA | Nyambiti | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | A |
| | BuzurugaMashariki | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | Ustawi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | BuzurugaKusini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| | Buzurugakaskazini | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/X | |
| BUSWELU | Kigala | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | B |
| | Bulola A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Bulola B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Zembwela | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Buhyila | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Bulolamlimani | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Bujingwa | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Majengomapya | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Buswelu | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| | Busenga | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XI | |
| KISEKE | Kabambo | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | B |
| | Kiseke | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| | Isenga | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| | PPF | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| NYASAKA | Nyasaka | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | A |
| | Kiloleli B | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| | Chamwenda | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| | Nyasaka | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| | Nyasaka Centre | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XII | |
| NYAMHONGOLO | Kashishi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XIII | C |
| | Iramba A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XIII | |
| | Mtakuja | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XIII | |
| | Bukumula | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XIII | |
| KAHAMA | | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XIV | C |
| BUGOGWA | Igombe A | LGA/159/2023/2024/NC/ 03//XV | C |
| | Lugezi | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XVI | |
| | Bugogwa | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XVI | |
| | Kigote | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XVI | |
| | Kayenzendogo | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XVI | |
| SHIBULA | | LGA/159/2023/2024/NC/ 03/XVII | C |

**MAELEZO KWA WAOMBAJI:-**

1. Muombaji lazima awe na leseni hai kwa ajili ya Utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajili wa kwenye VAT basi aonyeshe usajiliwa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney).
2. Dhamana kwa muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration)
3. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba na mtaa au kata unayoomba na yaelekezwekwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI,HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 MWANZA.**
4. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri, asiwe na historia yakusababisha migogoro ya aina yeyote.
5. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha na vifaa vya kukusanyia taka ngumu na ahakikishe kwamba vituo vyote vya kukusanyia taka ngumu ni visafi kipindi chote cha muda wa mkataba.
6. Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi 100,000, fedha ambazo hazitarudishwa.Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni.Maombi yote ya ambatishwe na picha mbili za passpoti size za hivi karibuni.
7. **Mwisho wa kupokea maombi ni 13/06/2023 saa 6.00 mchana, Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**

**MHANDISI MODEST J APOLINARY**
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Alichokibuni DC wa Korogwe 'Mamathon' kiungwe mkono

**UBUNIFU** wa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Jokate Mwegelo, hauna budi kuungwa mkono na watu wote ili kunusuru wajawazito na changamoto za uzazi.

Mkuu huyo wa wilaya ameanzisha mbio za wajawazito zenye lengo la kuondoa changamoto wanazokutana nazo wakiwa katika hali hiyo na vile vile kuwaweka katika afya bora.

Alipotangaza kuanza kwa mbio hizo, aliomba kinamama wenye hali hiyo kujitokeza na kujiandikisha kwa ajili ya kushiriki.

Kitu kilichotia moyo ni jinsi mwamko wa kinamama hao ulivyokuwa mkubwa na kufikia idadi ya wajawazito zaidi ya 2,000 waliojiandikisha.

Kilichopendeza zaidi ni jinsi kinababa nao walivyojitokeza kuwasindikiza kinamama hao katika mbio hizo.

Kwa kweli jambo hilo ni la kuungwa mkono na watu wote ili kulinda afya za wanawake wasikumbane na matatizo wakati wanapokwenda kujifungua.

Tumeelezwa kuwa wakati mbio hilo zikiendelea baadhi ya kinamama walikimbizwa hospitali baada ya kujisikia hali ya kutaka kujifungua.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, mwanamke anapokuwa katika hali ya ujauzito anatakiwa kufanya mazoezi ya mara kwa mara hasa ya kutembea, ili kupata urahisi anapofikia wakati wa kwenda kujifungua.

Mwili unapokuwa na mazoezi humsaidia mama kuondokana na shida zinazojitokea wakati anapokuwa na ujauzito.

Cha kuzingatia tu ni kwamba kabla ya kuanza mazoezi hayo ni lazima mtu afuate ushauri wa daktari ambaye atamwelekeza nini cha kufanya na nini asifanye.

Wakati DC akihamasisha mbio hizo, alisema wazi kuwa wajawazito wenye miezi ya karibu ya kujifungua hawashauriwi kushiriki katika mbio hizo kwa sababu mama anaweza akapata athari ikiwamo kujifungua kabla ya miezi kutimia.

Sisi tunampongeza DC Jokate kwa ubunifu huo na ameonyesha jinsi anavyowajali wanawake wenzake hasa ikizingatiwa kuwa na yeye amepitia katika hali hiyo na sasa ni mama.

Hamasa iliyoonyeshwa na kinamama hao pia ni kuunga mkono ubunifu wa mkuu wao wa wilaya na kujiweka katika mazingira yenye afya bora katika kipindi cha ujauzito.

Ushauri wetu ni kuwa ubunifu huu ulioanzishwa na Jokate uigwe pia kwenye wilaya na mikoa mingine ili tuwasaidie kinamama wanaopitia changamoto za uzazi.

Sio kitu kibaya kuiga mazuri yaliyoanzishwa na kiongozi mmoja, kwa kuwa hiyo itaonyesha kuwa jambo hilo ni zuri na linapaswa kuendelezwa.

Mwenyewe Jokate akishiriki mbio hizo alisema lengo la kufanya tukio hilo ni kuenzi yale yote ambayo Rais Samia ameyafanya kwa ajili ya kusaidia wanawake na watoto.

Pia, katika mbio hizo walitoa masharti kwa wale wenye ujauzito wa miezi kuanzia nane wasihudhurie kwa sababu wapo katika hali ya kujifungua wakati wowote.

Katika mbio hizo wajawazito pia walipewa ushauri wa vyakula bora wanavyotakiwa kula wakati wakiwa katika hali hiyo ili kujenga afya ya mama na ya mtoto aliye tumboni.

Kwa hiyo, mbio hizo sio tu zinamsaidia mama kwa mazoezi bali pia zinatoa elimu ya vyakula anavyotakiwa kula akiwa katika hali hiyo.

Tunarudia kumpongeza Jokate kwa ubunifu huo na kuzidi kumtia moyo wa kubuni vingine vizuri zaidi kwa sababu ameonyesha kuwa ni jembe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Somo la maadili shuleni lifanikishe kupunguza rushwa

**RUSHWA** ni adui wa haki, utu na heshima ya binadamu, vilevile vitendo vya utoaji na upokeaji rushwa, vimekuwa vikileta vilio karibu sekta zote, sehemu ya kazi na maeneo mengine ya kutolea huduma za kijamii.

Vitendo vya rushwa, ndivyo vinavyochangia kukwamisha shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja na jamii kwa ujumla, hivyo ni wazi kwamba rushwa ni adui wa haki, utu na heshima ya binadamu.

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anapofanya ukaguzi na kutoa taarifa kwa umma, upigaji mwingi wa fedha za umma umekuwa ukidhihirika, katika taasisi za umma.

Kushamiri kwa rushwa, kuna chimbuko lake ambalo ni mmomonyoko wa maadili unaoanzia katika ngazi ya familia hadi taifa. Hivyo, ninadhani vita dhidi yake ingeanzia shuleni kwa wanafunzi kufundishwa somo la maadili.

Mmomonyoko ndiyo unaozaa maovu, ikiwamo kuenea kwa rushwa ambayo imekuwa sugu katika maeneo mbalimbali na kusababisha jamii kukosa haki, huku baadhi ya watoaji na wapokeaji wakiichukulia kama jambo la kawaida.

Wakati jitihada za kupambana nayo zikiendelea, ni wakati mwafaka wa kuwa na mitaala, kwa ajili ya somo la maadili, ambalo linaweza kusaidia wanafunzi kuitambua rushwa wangali wadogo, athari zake na kuiona kama adui wa maendeleo.

Nimaamini kuwa kupitia somo hilo, wanafunzi wanaweza kujua rushwa ni nini, ikiwamo ya ngono, fedha na vitu vingine badala ya kuisikia tu bila kujua maana yake na madhara yake na kujikuta wakijiingiza humo.

Wanafunzi wakipata elimu kuhusu rushwa na madhara yake, watakapokuwa watu wazima wataendelea kuichukia, kutokana na ukweli kwamba inakwamisha maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

Hivyo, si vibaya ukawekwa mkakati maalumu wa kuanzisha somo hilo kwa shule za msingi hadi juu ili wanafunzi wapate elimu kuhusu rushwa, kwani ni miongoni mwa mambo ambayo yanachangia mmomonyoko wa maadili.

Ninaunga mkono juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa za kupambana na rushwa ikiwamo za kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni, ili wanafunzi wapate elimu ya madhara ya tatizo hilo.

Hatua hiyo ni nzuri kwa sababu inaweza kuandaa wanafunzi kupinga rushwa wangali wadogo hata pale wanapokuwa watu wazima waendelee kupambana nayo kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla.

Lakini, wakati vita hii ikiendelea, suala la kuwa na somo la maadili ninadhani ni la muhimu, kwani linaweza kusaidia wanafunzi kutambua mambo mbalimbali yanayohusiana na maadili mema.

Kama nilivyoeleza, taarifa za kila mwaka za CAG, zimekuwa zikionyesha ubadhirifu wa fedha za umma, ujenzi wa miradi duni na vilevile kukosekana heshima kwenye matumizi ya fedha za walipakodi ambao wengi wanalalamikia ukosefu na upungufu kwenye huduma, hivyo ni muhimu kuwapo mikakati mbalimbali ya kuwaandaa vyema wanafunzi ikiwamo somo la maadili.

Kwa kawaida, viongozi na watumishi bora wa umma, huandaliwa tangu mwanzo, hivyo kuanzisha somo la maadili shuleni linaweza kusaidia kuandaa viongozi watakaoleta mapinduzi chanya ya maendeleo ya nchi.

Utaratibu wa utoaji wa elimu kuhusu madhara ya rushwa kutolewa kuanzisha shule za msingi, ni mtazamo unaolenga kuhakikisha rushwa inaondolewa nchini kuanzia sasa na baadaye.

Maadili na uzalendo ni mambo yanayohitajika sana kujengwa upya na kuimarishwa ndani ya akili na mioyo ya watoto wa taifa hili kwa sababu kilichoziinua nchi kama China, Japan, Korea ni uzalendo na maadili hasa kufanyakazi.

# Makamba ataja vipaumbele 10 TPDC, TANESCO kujiendesha kibiashara

**Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, ametaja vipaumbele takribani 10 vya wizara katika kufikia malengo makubwa ikiwamo kuimarisha mashirika ya kimkakati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ili yafanye kazi kibiashara na kuchangia uchumi wa nchi.

Januari aliyasema hayo jana alipozungumza katika mtandao wa Clubhouse ulioandaliwa na Habari Maelezo zikiwa zimebaki siku chache wizara hiyo kuwasilisha bajeti yake wiki hii.

Alitaja kupaumbele cha pili ni kuleta matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia majumbani na viwandani kwa kuwa asilimia 85 ya inayotumika sasa ni biomass ambayo si salama kwa afya ya wanadamu na mazingira. Pia kusambaza gesi asilia nyumbani na viwandani.

"Kwa mara ya kwanza tumetoa vibali 20 vya kujenga vituo dada na mama vya kujazia gesi ili shughuli hiyo ishamiri," alisema January.

Makamba alitaja kipaumbele cha tatu kuwa ni kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, kupanua na kuongeza miundombinu ya usafirishaji wa nishati hiyo, kupanua usambazaji wake na kufikisha gridi ya taifa kule ambapo haijafika.

Kipaumbele cha nne kwa mujibu wa waziri huyo ni kufikisha umeme vijiji ili kuyafikia maeneo mengi zaidi, akitolea mfano kuwa kati ya vijiji 12,000 vilivyopo nchini 10,000 vimefikiwa huku vitongoji 28,000 vimefikiwa kati ya 64,000 na kuacha pengo la vitongoji 36,000.

Kipaumbele cha tano ni utekelezwaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa kuchakata na kusindika gesi iliyogunduliwa katika kimiminika, ili itumike nyumbani na nyingine isafirishwe katika masoko ya dunia.

Cha sita ni kuongeza matumizi ya nishati jadidifu ambapo kwa mara ya kwanza leo wizara hiyo itasaini mkataba wa kuingiza megawati 50 za umeme wa jua kwenye gridi.

Kipaumbele cha saba ni kuongeza usambazaji wa mafuta ya petroli ili kuwapo uhakika wa upatikanaji wa nishati hiyo nchini kwa kuwa ni mhimili wa shughuli za watu ,nane ni kuimarisha ushiriki wa sekta ya binafsi katika biashara ya nishati. Cha tisa ni kuhamasisha wazawa kuchangamkia fursa zilizopo katika wizara hiyo na kumi kufanya utafiti na utafutaji wa mafuta.

"Sisi tumebahatika kwamba eneo la nchi yetu lina maeneo mbalimbali yenye uwezekano wa kuwa na gesi na mafuta, ili mafuta hayo yapatikane lazima tufanye utafiti kwa kiwango kikubwa, eneo ambalo tumelifanyia utafiti ni asilimia 30 tu kwa hiyo kwa hiyo tutaongeza kasi hapo," alisema.

Alisema vipaumbele hivyo vimeongozwa na nyenzo wanazotumia kufanya kazi zake ambazo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa 2021-2025 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), maagizo na maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa husan sekta ya nishati pamoja na lengo namba saba la Maendeleo Endelevu linalosema upatikanaji wa nishati kwa wote.

Aidha alisema mradi wa umeme katika Bwawa la Julius Nyerere (JNHP) upo katika hatua za mwisho na mitambo ya awali itafanyiwa majaribio mwezi Aprili, 2024 na mpaka kufikia Juni mwaka huo umeme wa kwanza wa gridi utaingia kwenye gridi ya taifa.

# Shirika laongeza kasi utafiti matumizi nishati safi kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, shirika lisilo la kiserikali la utafiti wa nishati ya kupikia (TATEDO SESO), limeanza kuchukua hatua ya kuunga mkono juhudi hizo.

Hatua hiyo itawezesha kuokoa maisha ya Watanzania wanaopata athari za kiafya kutokana na matumizi ya kuni na mkaa pamoja na kuzuia uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji.

Akizungumza wakati wa mafunzo maalum ya teknolojia ya jiko sanifu lenye kupika kwa presha ya umeme kidogo kwa kamati za bunge za nishati, bajeti na wabunge rafiki wa mazingira kwenye ukumbi wa Pius Msekwa, Dodoma, Mkurugenzi Mtendaji wa TATEDO SESO, Mhandisi Estomi Sawe, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwezesha wabunge kupata elimu juu ya matumizi ya nishati hiyo.

Alisema elimu hiyo kwa wabunge itasaidia kusambaza teknolojia hiyo kwa wananchi, hivyo kuleta mabadiliko kutoka kwenye matumizi ya kuni na mkaa ili kulinda afya na mazingira.

Mhandisi Sawe pia alitoa rai kwa Watanzania kujenga utamaduni wa kutumia nishati ya umeme na kuachana na dhana kwamba ukipika kwa umeme, kuna gharama kwa kuwa utatumika mwingi.

Katika hatua nyingine, Sawe alipongeza jitihada za serikali katika kushirikiana na mamlaka za serikali na taasisi zinazohusika na nishati katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa mujibu wa Sawe, nchini Tanzania, zaidi ya wananchi milioni 55 hawatumii nishati na teknolojia za kisasa na safi za kupikia. Alisema hiyo ni zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wote ambao wanategemea kuni na mkaa. Kutokana na hali hiyo, alisema kuna umuhimu wa kuongeza kasi katika elimu na utafiti wa nishati safi ya kupikia ili kuokoa mazingira yanayoharibiwa kutokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Danstan Kitandula, alisema kamati yake itashirikiana na kamati ya mazingira na ile ya bajeti, kuishauri serikali ilifanyie haraka jambo hilo ili kuwafikia wananchi wengi kuondokana na mambo yanayohatarisha mazingira.

Pia alisema watafanya kila jitihada kushauri serikali kupunguza au kuondoa kodi ili wananchi wa kipato cha chini wanufaike na nishati ya majiko sanifu yanayotumia umeme kidogo.

Mbunge wa Mmchinga, Salma Kikwete, alipongeza jitihada za TATEDO SESO kubuni nishati mbadala na kutoa elimu kwa wabunge ili kuwezesha wananchi kujua tofauti kati ya matumizi ya kuni na nishati ya umeme ili kulinda afya zao.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

**MWALIKO WA ZABUNI**

**Tarehe: 30 May, 2023**

**ZABUNI NAMBA LGA/159/2023/24/NC/04 YA WAKALA WA UTOZAJI WA ADA ZA MAEGESHO YA VYOMBO VYA USAFIRI KWENYE HIFADHI ZA BARABARA KATIKA MANISPAA YA ILEMELA**

1. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inapenda kualika wazabuni ili waweze kuwasilisha zabuni zao kwa ajili ya kukusanya Mapato yatokanayo na ada ya maegesho ya vyombo vya usafiri katika hifadhi za barabara zilizoko ndani ya Manispaa ya Ilemela. Maeneo ya Halmashauri ambayo yametengwa kwa ajili ya Kutoza Ada za Maegesho ya vyombo vya usafiri ni yanasomeka katika Jedwali A Sehemu ya Tano;kwenye nyaraka ya zabuni hii.

2. Waombaji wanaalikwa kuwasilisha Zabuni zao kwa ajili ya kukusanya Mapato ya Ada za Maegesho ya vyombo vya usafiri kwenye hifadhi za barabara katika Manispaa ya Ilemela;

3. Waombaji wanatakiwa wawe wamekidhi vigezo na masharti yafuatayo:
   i) Mwombaji anatakiwa awe na ofisi ya kudumu anapofanyia kazi zake;
   ii) Awe na leseni hai ya biashara inayoruhusu kufanya kazi hiyo;
   iii) Aonyeshe mchanganuo wa maoteo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakacholipa kwa Taasisi Nunuzi kwa kila muda wa mwezi mmoja ndani ya mwaka mmoja;
   iv) Kuzingatia kuwa fomu ya maombi ya Zabuni inapaswa kujazwa na kusainiwa na mwakilishi halali wa Mzabuni mwenye Hati ya Kiapo cha Nguvu ya Kisheria (Power of Attorney) katika Zabuni hii kwa kampuni)
   v) Anapaswa kujaza na kuwasilisha tamko la dhamana ya zabuni lililoambatanishwa kwenye kabrasha la zabuni;
   vi) Anapaswa kuwasilisha orodha ya vifaa vya utendaji kazi, mahali ofisi ilipo (aoneshe endapo amepanga au anamiliki), idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao kama ilivyoainishwa kwenye majedwali katika kiambatisho 'A'; kwenye nyaraka ya zabuni hii.
   vii) Awasilishe dhamana ya utendaji kazi (Performance Security), katika muundo wa dhamana kutoka Benki (Unconditional Bank Guarantee) asilimia kumi (10%) au insurance bond ya asilimia kumi na tano (15%) ambayo itakuwa na thamani ya ya makusanyo ya Ada za Maegesho kwa mwezi, dhamana hiyo iwasilishwe ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kupewa barua ya kutunukiwa zabuni
   viii) Mwombaji napaswa kuwasilisha cheti cha Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN)/VAT na amesajiliwa kama mlipa kodi kwa mujibu wa Sheria za Tanzania na hajazuiliwa kupewa zabuni na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kujihusisha na shughuli za Ununuzi wa Umma;
   ix) Anapaswa kuwasilisha hati halali ya kuthibitisha ulipaji wa kodi ya mwaka 2022 (Tax Clearance Certificate);
   x) Awe tayari kutumia mfumo wa ukusanyaji wa Mapato wa Kielektroniki kulingana na maelekezo ya Halmashauri
   xi) Taasisi Nunuzi haitalazimika kukubali Zabuni yako, na ina haki wakati wowote ya kufuta mchakato kwa sababu za kisheria.
   xii) Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi 100,000 na fedha hizo hazitarudishwa.Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Maombi yote yaambatishwe na picha mbili za passpoti size za hivi karibuni.

4. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba na maombi yaelekezwe kwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI,HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ,S.L.P 735 MWANZA.**

5. Mwisho wa kupokea maombi ni 13/06/2023 saa 6;00 mchana,Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa Ushindani wa Kitaifa ulioainishwa kwenye Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, zikisomwa pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2016 na ziko wazi kwa waombaji wote wa hapa nchini.

**Mhandisi Modest J. Apolinary**
**Mkurugenzi wa Manispaa**
**ILEMELA**

# Gwajima afurahia huduma ya maji jimboni

**Na Joseph Mwendapole**

MBUNGE wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, amemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwatua ndoo wananchi wa jimbo la Kawe kupitia mradi mkubwa wa maji ambao umegusa maeneo mengi ambayo hayakuwa na maji.

Mradi huo wa maji ni wa Makongo Bagamoyo ambao ulizinduliwa hivi karibuni na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA).

Gwajima alitoa pongezi hizo wakati wa ziara ya Mwenge wa Uhuru ambao ulikagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya maji kwenye Jimbo la Kawe jijini Dar es Salaam.

"Hii ni neema kwa wananchi wangu wote, niwasihi wananchi kujitokeza kwa wingi kuomba maji kwa kufuata utaratibu sahihi uliowekwa na Serikali kwasababu Rais Samia ameonyesha kutujali sana kwa kutuletea mradi mkubwa kama huu ambao utaondoa kero ya maji," alisisitiza Gwajima.

Akizungumza wakati wa ziara ya Mbio za Mwenge 2023, kiongozi wa mbio hizo, Abdalla Shaibu Kaim, alisema mradi huo umebeba matumaini ya kupata maji kwa wananchi hivyo ni wajibu wa DAWASA kuhakikisha huduma inafika kwa kila mwananchi kwa kuwa mradi umeshakamilika.

Alisema mradi huo utanufaisha wananchi wa Mbweni, Bunju, Ununio na Boko na kwamba ameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo unaosambaza maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo.

"Huu ni mradi mkubwa na wa kimkakati ambao serikali imewekeza fedha nyingi kiasi cha bilioni 71 kwa lengo la kuhakikisha wananchi wote walengwa wanapata huduma ya majisafi kwa hiyo wananchi changamkieni maji na muutunze," alisema Kaim.


"Tumetembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, ni kazi kubwa imefanyika kupitia DAWASA, hivyo niwatake DAWASA sasa mhakikishe huduma ya maji inafika kwa kila mwananchi kupitia miundombinu hii iliyojengwa kwa fedha nyingi," alieleza.

"Napenda kumshukuru sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyowajali wananchi wake na kuelekeza bilioni 71 kutoka Benki ya Dunia zije hapa ili wananchi wote wapate huduma ya majisafi," alisema Kaim.

Naye Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema DAWASA imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye mikoa yote minne inayotoa huduma kila siku.

Alisema DAWASA imeendelea kusisitiza na kuchukua hatua mbalimbali za kulinda na kutunza vyanzo vya maji ikiwamo Mto Ruvu ili kuwezesha miradi hiyo mikubwa iliyokamilika ili iweze kutoa huduma kwa kipindi chote cha mwaka.

Mradi huo umekamilika na mpaka sasa DAWASA imefanikiwa kuunganisha wananchi 30,000 na huduma ya maji na lengo ni kuunganisha wananchi zaidi ya 60,000.



Watuhumiwa wa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kuteka, Hussein Mwinyijuma na Celestine Kamuli, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kuelekea mahabusu ya Ukonga, baada ya kusomewa mashtaka yanayowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanaodaiwa kupora simu kwa kutumia silaha kortini

**Na Grace Gurisha**

WAKAZI watatu mkoani Morogoro, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa tuhuma za unyang'anyi wa kutumia silaha na kumteka Hussein Mohamed kisha kumwibia simu aina ya IPhone.

Wakazi hao ni Sufiani Kideku (30), Celestine Kamuli (32) wote wakazi wa Kizuka, Morogoro na Hussein Mwinyijuma (47) mkazi wa Gairo Magengeni, Morogoro.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Ferdnadri Kiwonde, kuwa washtakiwa hao wanadaiwa kufanya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Mwanga alidai kuwa Mei 17, 2023 washtakiwa wakiwa eneo la Zaramo, mtaa wa Jamhuri ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, waliiba simu moja aina ya IPhone mali ya Hussein Mohamed.

Alidai kuwa kabla na baada ya kuiba simu hiyo, walimtishia Hussein kwa bastola aina Luger na walimteka mtu huyo kwa lengo la kuiba na kubaki na mali hiyo.

Baada ya washtakiwa kumaliza kusomewa shtaka hilo, walikana kuhusika na madai hayo na Wakili Mwanga alidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

**Wakazi hao ni Sufiani Kideku (30), Celestine Kamuli (32) wote wakazi wa Kizuka, Morogoro na Hussein Mwinyijuma (47) mkazi wa Gairo Magengeni, Morogoro.**

Hakimu Kihonde aliwauliza washtakiwa kama wana chochote cha kuzungumza na kudai kuwa hawana na kuwaeleza kuwa watakuwa chini ya ulinzi kwa sababu shtaka wanaloshtakiwa nalo halina dhamana.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Juni 12, 2023 kwa kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

## CCT yakoshwa na utendaji wa Samia

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT) Mkoa wa Morogoro imesema inaridhishwa na utendaji kazi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutokana na kuwarahisishia kazi ya kuhubiri upendo na amani.

Katibu wa CCT Mkoa wa Morogoro, Mchungaji Regnard Mdugo, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya Siku ya CCT inayofanyika kila mwaka kwa kuwakutanisha viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali wanachama wa jumuiya hiyo, yaliyofanyika katika viwanja vya Mashujaa mjini hapa.

Mchungaji Mdugo alisema kazi ya viongozi wa dini ni kuhubiri upendo na amani lakini kazi hiyo hushindwa kufanikiwa ikiwa viongozi wa kisiasa wataenenda kinyume cha matakwa ya wananchi ikiwamo katika kukabiliana na changamoto walizo nazo.

Alisema kasi ya utendaji kazi wa Rais Dk. Samia katika kushughulikia changamoto za wananchi kwenye maeneo ya elimu, afya, miundombinu na maji, inakata kiu ya Watanzania na kuwafanya kuwa wasikivu na watulivu hata wanapokuwa kwenye ibada.

"Jumuiya ya Kikristo (CCT) Mkoa wa Morogoro, inaridhishwa na kasi ya utendaji wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na tunaukiri ukweli kuwa anafanya kazi nzuri sana katika uongozi wake na kuwa amejikita katika kushughulikia matatizo ya wananchi kwa kuimarisha sekta za elimu, maji, afya na miundombinu," alisema.

Mchungaji Mdugo aliongeza kuwa hakuna ubaya kwa viongozi wa dini kusifu viongozi wa kisiasa pindi wanapoitendea vizuri jamii wanayoiongoza na vivyo hivyo ni kazi ya viongozi wa dini kukosoa ikiwa kukabainika mwenendo usioridhisha.

Mmoja wa washiriki wa maadhimisho hayo, Joseph Chuwa, alisema utendaji kazi wa Rais Dk. Samia unaendelea kuwa mwanga kwa jamii ya kitanzania katika kuimarisha amani na upendo uliopo nchini.

## DC azuia shughuli za kibinadamu milimani

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, ameagiza wananchi wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya milima iliyoko wilayani humo kusitisha mara moja kwa kuwa serikali itawachukulia hatua kali za kisheria.

Pia mkuu huyo wa wilaya ametaka wananchi hao kuchukua hatua hiyo itakayosaidia kuirejesha milima hiyo katika hali yake ya kawaida ili kupunguza athari zinazotokana na uharibifu huo ikiwamo ya mafuriko.

Emmanuela alitoa agizo hilo juzi alipotembelea maeneo yaliyoharibiwa na wakazi wanaozunguka mlima huo kwa kufanya shughuli za kilimo na kukata miti ya asili katika mlima Kivesi, Kata ya Sokon II katika Halmashauri ya Arusha, wilayani humo.

Aidha, alisema kutokana na shughuli hizo zimeleta athari kwa wananchi wengine wanaoishi matika maeneo ya bondeni.

Licha ya kutoa agizo hilo, pia aliwataka wananchi hao kuanza kuweka utaratibu wa kushuka mapema kutoka maeneo hayo kabla sheria haijaanza kuchukua mkondo wake.

"Tamko la serikali ni kwamba wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye milima yote ya Wilaya ya Arumeru, waanze kushuka na tushirikiane kwa pamoja kurejesha miti kwenye yale maeneo ambayo imekatwa," alisema Emmanuela.

Alisema kwenye milima yote iliyoko katika wilaya hiyo, kuna mipaka ambayo imewekwa na serikali, haruhusiwi kwa mtu yeyote kuvuka mipaka hiyo.

"Kuanzia sasa hivi naamuru kwa ambao wamevunja utaratibu huo kusitisha kufanya shughuli zozote za kibinadamu kwa kuwa kufanya hivyo ni kuvunja sheria za nchi," aliongeza.

Baadhi ya wakazi wanaozunguka maeneo ya mlima huo, wameiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wanaovuka mipaka iliyowekwa ili kusaidia utunzaji wa mazingira hata kwa vizazi vijavyo.

"Kwa kweli uharibifu ni mkubwa kuna watu wanaovuta magogo na kusababisha maji mengi kutiririka kuelekea kwenye makazi ya watu, ninaiomba serikali kuchukua hatua wasitishwe kuingia kwenye misitu wa asili na wabaki kwenye sehemu zao tu," alisema mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Ng'iresi, Kata ya Sokoni II, Maglan Lukumay.

Awali, baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, walikumbwa na mafuriko yaliyosababisha upotevu wa mali za wakazi hao, huku wengine wakikosa makazi hasa msimu wa mvua za mwaka huu.

Kutokana na kutokea kwa madhara hayo, imesababisha mkuu huyo wa wilaya kutembelea eneo la mlima Kivesi ambalo liadaiwa kuwa chanzo kikubwa cha mafuriko hayo pamoja na kuangalia uharibifu.

# 'Maadui wa viumbe hai ni uchafu wa plastiki'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wakristo Tanzania (CCT), Dk. Fredrick Shoo, amesema utafiti umeonyesha kuwa maadui wakubwa wa mimea ardhini na viumbe vya baharini ni taka za aina za plastiki zinazotupwa.

Dk. Shoo, ambaye ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), amewataka Watanzania kutokomeza plastiki ili kuwapo kwa usalama zaidi.

Aliyasema hayo jana wakati akikabidhi nguo za watoto wachanga ikiwamo mablanketi pamoja na vifaa vya shule kwa watoto wagonjwa na wajawazito waliojifungua katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi.

Alisema, kuna umuhimu kwa kila Mtanzania kutunza mazingira kwa kukataa plastiki na kupanda miti mitatu hasa katika msimu huu wa mvua za masika.

Vilevile, alisema umefika wakati kwa serikali kuanzia ngazi za vitongoji hadi taifa, kushirikiana kutokomeza plastiki kwa ajili ya usalama wa Taifa la Tanzania.

"Moja ya vipaumbele vya jumuiya hii ni kutokomeza taka za plastiki pamoja na kutunza mazingira kwa ustawi wa binadamu na viumbe wanaoishi baharini na nchi kavu, tunaomba wananchi wote kupinga suala hili kama sehemu ya maisha yetu.

"Pia, tumeotesha miti kama ishara ya kuonyesha jumuiya hii inatilia mkazo jambo la utunzaji na uhifadhi mazingira, ili kupeleka ujumbe kwa kila mtu hivyo kuna haja kila Mtanzania aone umuhimu wa kutunza mazingira na uumbaji wa Mungu na mwaka huu tumejipanga kutokomeza plastiki," alisema Dk. Shoo.

Akizungumzia utoaji wa misaada hiyo, alisema wametoa kwa makundi hayo kuonyesha alama ya upendo kwa wahitaji.

"Tumekuja hapa kama jumuiya ya Wakristo Tanzania ambayo ina makanisa wanachama 12, tumefika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi, kama sehemu ya kuwashirikisha wagonjwa wa hospitali hii na wajawazito na waliojifungua tumeleta nguo za watoto, mablanketi ikiwa zawadi kutoka kwenye jumuiya yetu."

Pia alizungumzia mmomonyoko wa maadili kuwa sio wakati wa kurushiana lawama badala yake aliwataka wazazi kusimamia malezi ya watoto ili wawe wenye hofu ya Mungu.

"Wakati wa kulaumiana umekwisha, wazazi watambue familia ni kiwanda cha kuzalisha maadili na tufanye mambo yaliyokuwa mema kuwa na kizazi chenye ubora," aliongeza.

Naye Katibu Mkuu wa CCT, Mchungaji Kanoni Matonja, alisema kwenda katika hospitali hiyo, kutoa msaada huo kwa makundi hayo ni kama zawadi ikiwa ni ishara ya kurudisha sehemu ya walichojaliwa katika jamii.

Katibu wa hospitali hiyo, Rose Maufi, akipokea msaada huo, alisema kitendo cha CCT kuwakumbuka wagonjwa hao ni ishara ya upendo kwa kuwatia moyo watumishi wa afya hasa wa Hospitali ya Mawenzi.

Mmoja wa kinamama waliopatiwa msaada huo, Mary Msuya, ameushukuru uongozi huo kwa kutoa zawadi na waliomba ili kukabiliana na matatizo ya uzazi.

"Tunawashukuru kwa misaada yenu, kila mara endeleeni kuwaombea wajawazito na watoto wachanga wanaokabiliwa na matatizo mengi hasa ya afya, kiuchumi na kijamii," alisema Mary.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga (kulia), Waziri Kindamba, akikagua kizimba cha wafanyabiashara wa samaki katika soko kuu la Wilaya ya Pangani juzi, (kushoto) ni kiongozi wa timu ya wakaguzi wa mradi huo, Timotheo Sosiya. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

## Askofu aiomba jamii kuendelea kusimamia maadili

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, ameiomba serikali na jamii kuendelea kusimamia mila na desturi nzuri ili kulinda utamaduni ambao utasaidia kuepukana na mmomonyoko wa maadili ulioibuka siku za hivi karibuni.

Konki alitoa ombi hilo jana katika ibada ya shukrani aliyoifanya kanisani hapo, akishukuru kwa kuchaguliwa tena kuliongoza kanisa hilo, katika uchaguzi uliofanyika Desemba 29, mwaka jana.

"Mila nzuri ziendelezwe na yale mabaya yaachwe mfano yale tuliyofundishwa kutokuoa ndugu zetu ilikuwa vizuri kwa kuwa ilikuwa kinyume na utamaduni wetu," alisema Konki.

Aidha, alisema misingi ambayo imewekwa na wazee wa zamani ilikuwa mizuri kwa kuwa waliambiwa wasioe ndugu zao.


Aliiomba serikali kusimamia vizuri matumizi ya mitandao ya kijamii ili kuepusha watu kujifunza tabia chafu za kimagharibi kama za ushoga.

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Calvary Assembly of God, Dunstan Maboya, alisema tatizo lililoko kwa viongozi wa serikali wanaofuja mali za umma linasababishwa na makuzi na malezi mabaya waliyolelewa toka wakiwa vijana.

"Tukipoteza miiko tunapoteza utu hata kama serikali wakijenga magereza nyingi hazitasaidia Mungu tu ndio anaweza kumbadilisha mtu," alisema Maboya.

Kuhusu viongozi wa dini wanaobaka, kulawiti au kuwafanyia ukatili watoto wachanga wa mwaka mmoja au mitatu, alisema hao wanakuwa wameingia kwenye utumishi ila hawana wito.

"Anayefanya kinyume na maadili kwa watoto kwa kuwanyanyasa huyo anakuwa hajaitwa na Mungu," alisema.



# Wananchi 7,000 waondokana matumizi maji yasiyo salama

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

ZAIDI ya wananchi 7,000 kutoka katika Kijiji cha Lukindo na Kishenge, Kata ya Katoma, Halmashauri ya Wilaya Bukoba mkoani Kagera wameondokana na adha ya kusubiri maji ya chemchemi kwa muda mrefu ambayo pia sio salama kwa afya zao baada ya kusogezewa huduma hiyo na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Wakizungumza na Nipashe iliyotembelea kijiji hicho hivi karibuni, wananchi hao walisema kabla ya kujengewa ghati za maji karibu yao walilazimika kutafuta huduma hiyo katika vyanzo mbalimbali ambavyo sio salama ikiwa ni pamoja na chamchemi ambazo ziliwalazimu kusubiri kwa muda mrefu maji kutoka.

"Licha ya maji hayo kutoka kwa kiwango cha chini, lakini bado ilitulazimu kupanga mstari wa kusubiri huduma hiyo kwa zaidi ya siku nzima ambayo hata hivyo maji yake hayakuwa salama kutokana na kutokutibiwa," alisema Esta Godwin, mkazi wa kijiji hicho.

Aileth Justus ni Mkazi wa Kata ya Katoma, alisema ilifikia wakati unazuka ugomvi na kusababisha hasara ya vyombo kupasuka pindi maji yanapoonekana kuwa kidogo na watu ni wengi.

Mjumbe wa chombo cha watumia huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO), Evance Innocent alisema, kulikuwa na mazingira magumu ya kupata maji kwa wananchi na sasa ujio wa miradi ya ghati ya RUWASA imesaidia kudhibiti adha hiyo na sasa wananchi wanaendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii wakiwa na uhakika wa kupata maji kwa wakati.

Alisema, matangi hayo husambaza maji katika maeneo ambayo yamejengwa magati ya kuteka maji na kufanya wananchi kutotumia muda wao mwingi katika shughuli ya maji pekee.

Alisema, huduma hiyo hutumiwa na wananchi 7,000 ikiwa wanamume ni 3,492, wanawake 3,801 wanaoishi katika kata hiyo ya Katoma.

Naye Meneja RUWASA wilayani Bukoba, Mhandishi Evarsto Mugaya, alisema kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa kwa wakala hao kumekuwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni tatu na kuongeza hali ya upatikanaji wa maji 68 mpaka 74 kwa mwaka 2019.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita (kulia), akizungumza na Naibu Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Melissa McNeil Barrett, alipofika ofisini kwa mkuu huyo wa wilaya mwishoni mwa wiki, kujadiliana kuhusu ustawi wa mtoto wa kike na mwanamke, katika jitihada za kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya makundi hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yabaini madarasa kujengwa chini ya kiwango

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imebaini ujenzi wa vyumba viwili ya madarasa katika Sekondari ya Bunambiyu wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga kujengwa chini ya kiwango na kutaka kurudiwa ili kuepusha madhara kwa wanafunzi.

Vyumba hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 40 havikusimikwa vizuri kwenye kuta zake pamoja na dari, koplo za madirisha zilionekana kupinda na madirisha ya aluminiam kutowekwa vizuri katika sehemu zake badala yake yamekandikwa saruji juu hali inayohatarisha watumiaji.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa TAKUKURU mkoani Shinyanga, Donasian Kessy, wakati akitoa taarifa ya ukaguzi na uchunguzi uliofanywa na taasisi hiyo kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha (2022/2023), kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Kadhalika, alisema walibaini kuwapo na vyufa kwenye baadhi ya madirisha pamoja na mikanda ya bodi kuachia nyufa na kutoa wito kwa wasimamizi wa ujenzi wa miradi ya maendeleo watekeleze wajibu wao ipasavyo na kuhakikisha majengo yanajengwa wa ubora unaotakiwa na kuendana na thamani ya fedha. Katika hatua nyingine, alisema taasisi hiyo ilidhibiti mianya ya rushwa katika ugawaji wa pembejeo pamoja na mbolea za ruzuku kwa wakulima katika Manispaa ya Kahama, ambako baadhi ya wakulima walikuwa wakisajiliwa mara mbili na walioandikishwa hawapewi taarifa zozote za kupata ruzuku ya mbolea.

Alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kuendelee kutoa taarifa za viashiria vya rushwa kwenye ofisi zao ambazo zipo kila wilaya mkoani humo kwa kupiga simu ya bure 0738-150196.

## Utekelezaji wa miradi wafadhili watakiwa kuwekwa wazi

**Na Timothy Itembe,** MARA

SERIKALI mkoani Mara imezitaka taasisi pamoja na mashirika mbalimbali kubainisha na kuweka wazi bajeti ya fedha za wafadhili zinazotolewa kutekeleza miradi ya kimaendeleo kwa kueleza watoaji wa fedha hizo na dhumuni ili kuepukana na ubadhirifu pamoja kuingiza nchini tamaduni zenye mrengo hasi.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Michael Mtenjele, wakati wa kikao cha tathmini ya mwaka 2023 wa shirika lisilo la kiserikali la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) na kueleza kuwa lengo la kufanya hivyo ni kuifanya serikali kutambua miradi ya mashirika inayotekelezwa, bajeti yake sambamba na madhumuni yake katika jamii.

Alisema kuwa hatua hiyo inakuja kutokana na baadhi ya asasi za kiraia hapa nchini kufutiwa usajili wake kutokana na kukiuka matakwa ya kisheria katika utendaji kazi na kuwataka kuungana na serikali pamoja na wadau mbali mbali katika kupinga vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto ikiwa ni pamoja na ukeketaji.

Ofisa wa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Tarime, Antoni Nyange, alisema tatizo la ukatili katika halmashauri hiyo limekuwa likitokana na wanawake kumiliki fedha hususani zile zinatokana na mikopo ya asilimia 10 na kuwafanya baadhi ya wanamume ambao baada ya baadhi ya machimbo kumilikishwa wakakosa ajira kuhitaji fedha hizo kuzitumia katika mambo yao binafsi.

Mkurugenzi wa Shirika la CDF, Konshuma Mtengeti, alisema wameanzisha mpango wa kushirikisha jamii dhidi ya mapambano ya ukatili kwa wanawake na watoto pamoja na serikali katika kila hatua ya utekelezaji wa mpango huo.

Akieleza adha wanazokumbana nazo katika kutoa maamuzi ya kesi za ukatili, Hakimu Mkazi, Vincencia Balyaruha, alisema wanapata wakati mgumu hususani katika kupata ushahidi kutokana na watoto kutishwa ama kukataa mtuhumiwa mahakamani licha ya kuwa hapo awali alikiri kutendewa kosa hilo na aliyeletwa mahakamani.

Kadhalika, alisema kuwa katika Sheria za Tanzania hakuna kifungu kilichobainisha kosa la ukeketaji ili kumtia hatiani mtuhumiwa badala yake wanatumia vifungu vya makosa ya jinai kuamua kesi hizo.



Ukurasa 12

Wananchi Dar wanapokusanyika darasani kujihoji tumefeli wapi?



Ukurasa 13

Khadija Nyangura mwanamama shujaa mapambano VVU, UKIMWI


Nipashe

# TESA

Jumanne Mei 30, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

## Juhudi za SBL, kuendeleza utalii, kuanza kugusa wasomi elimu ya juu


ELIMU
NA MWANDISHI
WETU


# Wazazi fanyeni 'homework' hizi wakati huu wa likizo

WAZAZI na walezi wanasubiri watoto warudi nyumbani wakati huu wa likizo inayoanza wiki hii Jumatano Mei 31, ni kipindi cha mapumziko chenye mambo mengi ambayo yanatakiwa kuyazingatia na kikubwa ni ulinzi, usalama na kusimamia mwenendo mwema.

Unapowakaribisha watoto kupumzika angalia ulichofanya muhula wa kwanza wa masomo unaokwisha, ndiyo muda wa kufuatilia maendeleo ya wanao shuleni pia weka msisitizo kwa wanaotarajia kufanya mitihani ya darasa la nne na la saba mna kidato cha nne ambao wengi wanabakia shuleni.

Ndiyo muda wa kufuatilia hatua kwa hatua maendeleo na kufahamu mafanikio na changamoto za kielimu kuanzia Januari hadi Juni ambazo wewe mzazi au mlezi hukutimiza wajibu wako.

Kuna baadhi hawaangalii wala kufuatilia daftari za watoto wenu kujua kuwa wameandika kazi za darasani na zile za nyumbani. Mtoto wako atafanikiwaje kufanya vizuri mtihani wa darasa la nne au la saba ama kidato cha nne kama haandiki notisi darasani, hafanyi mazoezi, hana vitabu, hujui habari za 'home work' na bila kujali kuwa ni wajibu wako kufuatilia?

Kama kuna walioko hivyo kuanzia sasa waamke na kuanza kutimiza wajibu huo wa usimamizi. Wapo wengine hawafahamu maana ya 'home work' au kazi za kufanyia nyumbani wala hawawasaidia watoto wao badala yake



Watoto wafunzwe kupika wakati wa likizo na kujengewa ujuzi wa mambo ya maisha. **PICHA: MTANDAO**

wanawaachia wafanyakazi wa nyumbani ambao wengi hawakufaulu wala kufanya vizuri kwenye masoma au unaligeuza kuwa jukumu la ndugu unaoishi nao, kuanzia sasa ni vyema kuachana na mienendo hiyo na kuwajibika.

Ni vizuri kuzingatia majukumu na muhimu pia kwenda shuleni na kukutana na walimu kufuatilia maendeleo ya watoto kwa muhula na hata kwa miaka yote ili ufahamu changamoto, maendeleo na kushauriana la kufanya ili kupunguza matatizo.

### VUNJA MIIKO

Pamoja na watoto kupata muda wa kupumzika na kujiweka pembeni na mambo ya elimu na kupata wasaa wa kupumzisha vichwa na kujifunza vitu vingine vya kijamii. Wanaweza kwenda vijijini na hata mbali na nyumbani kuwatembelea ndugu na jamaa. Hata hivyo wakumbusheni watoto kuhusu maadili mema kuna wimbi la ngono za jinsia moja, ulawiti, ubakaji, ngono miongoni mwa watoto.

Aidha, watoto kuangalia picha za ngono kwenye mitandao ya simu, kompyuta na kwenye runinga za vibanda umiza. Wazazi, walezi na jamii wasikae kimya wafuatilie popote watoto walipo kufahamu wanachofanya.

Watoto waambiwe ukweli kuhusu kujamiiana watu wa jinsia moja, hatari inayowakabili, matumizi ya dawa za kulevya, bangi na mambo yote yanayowaathiri leo. Mzazi au mlezi ukikaa kimya usizungumze na watoto wako kwa vile ni mwiko kwa wazazi au walezi kuongea mambo hayo utaumia zaidi kwa vile watayasikia kwa marafiki na huko ndiko kupotezwa.

Ni vyema kutafuta wataalamu wakufundishe mbinu, lugha na njia bora ya kuwaeleza watoto kuhusu kujamiiana, mimba za utotoni, mahusiano ya jinsia moja, dawa za kulevya, bangi na athari za teknolojia kwenye kuwafundisha mambo ya mmomonyoko wa maadili kama ushoga.

Watoto wanapokuwa nyumbani wafundisheni kazi, hata huko vijijini waendako wafunzwe kufua nguo zao kuanzia sare na soksi, kadhalika wafue viatu hasa raba kwa kuwa wanasoma wanatakiwa kufahamu kujitegemea.

Nyumbani wanapokaa wafundishwe kutoa vyombo mezani na kuviosha, kusafisha nyumba, viwanja, bafu na hata kuwalisha wanyama wasidekezwe na kuachwa wakitazama runinga na kazi zote zikifanywa na watumishi wa ndani, kumbuke mtoto huyo anaandaliwa kuwa baba, mama wa kesho lakini pia ndiyo viongozi na raia bora wa taifa.

### KUWAAMINI WATOTO

Mara nyingi watoto wa shule za sekondari na msingi wanaonekana usiku wa manane kwenye maeneo ya starehe kama ndani ya disko, baa, kwenye mikesha ya harusi na pia kwenye maeneo yanaponywewa pombe za kienyeji. Jamii inajiuliza wamefikaje huko?

Jawabu ni kwamba wazazi na walezi hawakumbuki kufuatilia mienendo nyumbani hasa nyakati za usiku. Kumbukeni msiwaachie watoto funguo usiku. Funga milango na utunze funguo kama una wasiwasi na mienendo yao jitahidi kulala mapema kuanzia saa 3 ili uanze kufunga ifikapo saa 5:00 na ukae na funguo kama ni

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Wananchi Dar wanapokusanyika darasani kujihoji tumefeli wapi?

• Ni janga mporomoko wa maadili mitaani

KUWAPO kwa mmomonyoko wa maadili miongoni mwa Watanzania kuanzia kwenye familia na taasisi mbalimbali za umma na binafsi ni mojawapo ya sababu zinazotajwa kuchangia kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuashiria uwezekano wa kuwa na taifa lisilo na mwelekeo wala hatima bora siku zijazo.

Hofu hiyo, inawaamsha wadau mbalimbali kujitosa kushirikiana na serikali kufanya kila jitihada ili kusaidia kurudisha jamii kwenye mstari kwa kufuata maadili mema, miongoni mwao ni shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization ambalo hivi karibuni linawakusanya wazazi na walezi na kuwapa mafunzo ya jinsi ya kusimamia malezi bora ndani ya jamii na familia.

Shirika hilo linalojishughulisha na masuala la jinsia, likiwa na maskani Kitunda jijini Dar es Salaam, linawakutanisha wazazi na walezi wa kata hiyo ili kuwapa elimu ya malezi, anasema Mkurugenzi Prisca Ngweshemi.

Anaeleza kuwa kama ulivyo mmomonyoko wa madili, katika maeneo mengine ya Dar es Salaam na mikoa mingine hata Kitunda nako lipo tatizo hilo kuanza kulikabili.

"Himiza Development Organization ni mdau wa malezi, tumeitisha mafunzo ili kufanya sehemu yetu ya kulinda maadili katika maadhimisho ya wiki ya familia ingawa iliisha Mei 15 hali ya mmomonyoko ipo na inahitaji tiba," anasema Prisca.

Anaeleza kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni nzuri tena ni vyema watu kufunzwa na kujifundisha lakini kinachojiri leo imetumika vibaya kwa kusambaza picha za ngono kupitia mitandao ya kompyuta, simu kwenye makundi ya Whatsapp.

"TEHAMA inasaidia kuperuzi mambo ya masomo, lakini vijana wadogo wanaangalia mambo yasiyolingana na umri wao na kujikuta wakifanyiana au kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na uharibifu wa maumbile yao," anaonya.



Wazazi na walezi wakifuatilia mafunzo, tafakarini na mipango.
**PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Anasema vitendo hivyo vya ukatili kama kulawiti, kubaka, hufanyika majumbani, mitaani na hata shuleni, na kwamba chanzo kikubwa ni uduni wa malezi bora unaosababisha wajiingize katika vitendo hivyo bila kugunduliwa wala kuonywa na wazazi, walezi au jamii.

Anataja njia mojawapo ya kusimamia malezi hayo kuwa ni wazazi na walezi kufuatilia mienendo ya watoto wao, kujua marafiki zao na pia kutowanunulia simu kwa kuwa zinaweza kuwaingiza mtegoni.

Prisca anasema hatua hiyo iende sambamba na kutenga muda wa kukaa na watoto wao, kwa maelezo kwamba wazazi na walezi wa siku hizi wanatafuta mali zaidi na kuacha watoto wakijilea wenyewe.



Mkurugenzi wa Himiza Development Organization, Prisca Ngweshemi, akitoa elimu ya malezi bora kwa wazazi na walezi wa Kitunda.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa wakiwa na utaratibu huo, watasaidia kuepuesha watoto wao na wanafamilia kuingia katika mmomonyoko wa maadili na kujikuta wakiwa taifa bovu la baadaye.

"Mtoto anaweza kuwa na tabia njema nyumbani, akiwa mitaani ana mienendo tofauti hata shuleni akiwa tabia nyingine, hivyo kuweni karibu na walimu ili mjue uhalisi na nyendo za watoto wenu," anasisitiza Prisca.

Anasema bila kuzingatia hayo, mtu unaweza kuambiwa matendo mabaya ya mtoto wake akashangaa, kwa maelezo kwamba wapo wanaobadilika tabia kulingana na maeneo waliyopo na marafiki au watu wanaokutana nao.

**KUJIHESHIMU**

Wakati hali ikiwa hivyo kwa vijana wadogo, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo Zena Mtauka, anawataka wazazi na walezi kujiheshimu, akieleza kwamba baadhi yao wanachangia kuharibu mienendo na tabia za wengine wakiwamo watoto wao.

"Baadhi ya wazazi na walezi wakiwamo kinababa na kinamama, wanachangia kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili kwa kufanya ngono iwe na mabinti au wavulana ambao ni wadogo tena ni watoto wao wa kuwazaa," anasema Zena.



Watoto wafunzwe kupika wakati wa likizo na kujengewa ujuzi wa mambo ya maisha. **PICHA: MTANDAO**

## Wazazi fanyeni 'homework' hizi

**INATOKA UK.11**

kwenda uwani waambie wakuamshe uwasindikize kama huduma iko nje. Usiwaachie ufunguo maana wanafanya mambo mengine usiku bila familia kufahamu.

**KUJALI AFYA**

Wazazi na walezi unene kupindukia si afya, kwa mfano baadhi ya watoto wanaosoma katika sekondari hasa zile za kulipia wanakuwa wanene kupindukia. Wanakunywa soda hata nne, wanakula kuku zaidi ya mmoja kwa siku na wazazi au walezi wamelikubali na kuliendeleza hilo.

Huko si kumsaidia mtoto kwanini aruhusiwe kula 'chokleti', pipi au chochote. Dhibiti ulaji wa vyakula duni kama chips na kuku, zuia unywaji wa vinywaji baridi vyenye kemikali za kila aina kuanzia soda, cola si jambo jema kwa afya za watoto. Kwanini mwanao anenepe na kuwa na zaidi ya kilo 80 tena yuko darasa la nne na umri wake ni miaka 10. Pengine katika umri huo anatakiwa asizidi kilo 30 uliza wataalamu, si jambo jema, kumbuka bado ni mdogo usimnenepeshe kupindukia.

Usimwendekeze, fahamu ya kuwa huu siyo muda mzuri kuwadekeza watoto kupindukia ukiwapa kila kitu wanachotaka.

Wakati huu wazazi na walezi waandalieni watoto likizo yenye mafanikio kwa kuwapa chakula, mavazi, malazi lakini pia wapewe kazi za kufanya kuanzia kusoma masomo ya ziada au tuition, kuosha vyombo, kusafisha mazingira na kushirikiana na wenzao mitaani kucheza, kusali kwenye ibada ila usisahau muda wote kuwafuatilia.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Khadija Nyangura mwanamama shujaa mapambano VVU, UKIMWI

KHADIJA Nyangura ni mwelimishaji na mshauri nasaha katika hospitali ya mji wa Babati mkoani Manyara, anayepokea tuzo ya wapambanaji vinara kutokana na kazi kubwa ya kuelimisha jamii hasa ya wanaoishi na VVU ili kuendelea maisha bila kukata tamaa, kujiamini na kusonga mbele.

Ni miongoni mwa wanawake saba waliotunikiwa Tuzo ya Wapambanaji Vinara Champion Award na ya heshima 'honorary award' na Asasi ya Kiraia ya Wanawake Wanaoishi na VVU na UKIMWI (DWWT).

Tuzo hizo zinatolewa hivi karibuni na Baraza la Taifa la Watu Waishio na Virusi Vya Ukimwi (NACOPHA), jijini Dar es Salaam, kuenzi mafanikio na kazi nyingi ambazo wanawake na wasichana wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi walizofanya kwenye jamii na kuleta mabadiliko na kusaidia baadhi ya sheria kubadilishwa, akiita tuzo ya F.I.E.R.C.E ikimaanisha ujasiri, uhamasishaji, uwepesi, ustahimilivu na uwezeshaji.



Khadija Nyangura (kushoto), akipokea tuzo kutoka kwa Mratibu wa TACAIDS Dar es Salaam, Grace Kessy. **PICHA: DWWT**

Khadija anasema amepata tuzo kwa ajili ya kufundisha watoto wa shule za msingi na sekondari katika wilaya ya Babati akitembelea shule 11, kati ya hizo za msingi ni sita na sekondari ni tano alikoleta mabadiliko kwa watoto shuleni.

"Hivi sasa watoto wengi wanaoishi na VVU na UKIMWI wanahudhuria masomo, tofauti na miaka ya nyuma. Wakati wa mafunzo shuleni, nilitoa elimu kuanzia VVU, UKIMWI, unyanyapaa, afya ya uzazi, matumizi sahihi ya kondomu, hasa shule za sekondari na masuala ya ukatili wa kijinsia kwa watoto."

Anongeza: "Baada ya kutoa elimu shuleni, hivi sasa watoto wanaoishi na VVU na UKIMWI wengi virusi vimeshuka chini, wanasoma vizuri, najivunia kuwa sehemu ya mabadiliko hayo kwa sababu wanatumia dawa kikamilifu na hawezi kuwaambukiza wengine."

Mbali na hilo, ametoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa kwa wazazi na walezi ambao wanaishi na watoto WAVIU na kwa sababu hawawapi watoto dawa kwa usahihi endapo VVU vinaongezeka," anasema.

Khadija anasema amefikia ndani ya familia kuzielimisha kuhusu upimaji wa VVU na UKIMWI na kwamba alianza kazi ya kuelimisha tangu 2006 baada ya kupimwa na kugundulika kuwa na maambukizi ya VVU.

"Wakati huo, watu walikuwa hawataki kujitokeza kupima, mimi nilikuwa mfano wa kuigwa baada ya kugundulika na maambukizi na hatimaye nikajiweka wazi kwenye jamii, anakumbusha.

Anaongeza: "Nilikuwa natoa elimu kwenye mikutano ya hadhara na kusema kuwa ninaishi na VVU na mwaka 2007 nilitoa elimu ya unyanyapaa na maambukizo kupitia redio, televisheni, magazeti ya FEMA na watu wengi walianza kujitokeza kupimwa na kutambua hali zao."

Ilipofika 2010, alipata mafunzo ya Huduma za VVU na UKIMWI katika jamii na kuendelea kufundisha, kuwashauri wenzake walioacha dawa warudi kwenye huduma na tiba na kwamba ilipofika 2014, alipata mafunzo ya msaada wa sheria 'paralegal ' na akawa msaidizi wa kisheria kwa watoto.

## MAFANIKIO

Khadija anajivunia kupima vijana wanaoishi katika mazingira hatarishi zaidi ya 500, kati ya hao 30 walibainika na maambukizi na baadaye aliwaelekeza kwenda kwenye hospitali za rufani Babati kupata tiba na matunzo.

Anaushukuru Mtandao wa DWWT kwa kutambua kazi yake na kuahidi kuendelea kuelimisha watoto wengi zaidi na jamii katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mwenyekiti wa DWWT, Debora Enock, anasema tuzo hiyo inatolewa kutambua nguvu za wanawake na wasichana katika mapambano ya VVU na UKIMWI katika kuanzia kinga, tiba na matunzo.

"Kupitia mipango yetu mbalimbali, tumekuwa tukijitahidi kuwapa wanawake zana, rasilimali na mafunzo kama ya afya ya uzazi, haki za binadamu, ukatili wa kijinsia, unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya wanawake waishio na maambukuzi ya VVU, matumizi sahihi ya dawa na elimu ya ujasiriamali, afya ya akili na mazingira ili kufikia uwezo wao kamili." Anasema Debora.

Anasema wamejitahidi kwa ujasiri kufuatilia ndoto zao na kuokoa maisha ya wanawawake na wasichana wengine licha ya changamoto zote wanazokumbana nazo katika utekelezaji wa afua za UKIMWI.

Anasema DWWT ni asasi ya kiraia iliyosajiliwa Tanzania Desemba 2018 kutoka ofisi yake ya Kanda ya Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake Waishio na VVU Ukanda wa Afrika Mashariki (ICWEA).

> Wakati huo, watu walikuwa hawataki kujitokeza kupima, mimi nilikuwa mfano wa kuigwa baada ya kugundulika na maambukizi na hatimaye nikajiweka wazi kwenye jamii, anakumbusha.

## SAUTI YA TACAIDS

Mratibu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS Mkoa wa Dar es Salaam, Grace Kessy, anasema Tanzania inahitaji kuongeza juhudi zaidi kwani inakabiliwa na changamoto za UKIMWI ambazo zinahitaji kujibiwa kwa umakini na ujasiri, kuhamasisha jamii nzima kuhusu umuhimu wa kupima VVU, kuwahimiza watu kufanya maamuzi sahihi na salama, na kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma katika kupata huduma za afya.

Anasema pia wanahitaji kujenga mazingira ya upendo, uelewa na kutokuhukumu ili kuvunja unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI, akiwahimiza wasichana ambao ni nguvu ya taifa kuwa mabalozi wa mabadiliko.

"Ninyi ni kizazi kilichobeba matumaini ya taifa letu na mnaweza kuleta mabadiliko makubwa katika kupambana na UKIMWI. Jitahidini kuelimisha wenzenu, kuwa na mazungumzo ya wazi na familia na marafiki, na kuhakikisha kuwa mnazingatia na kulinda afya yenu wenyewe," anasema Grace

Mbali na hilo anaongeza: "Ninaamini wanawake tunaweza kufanikiwa katika kupambana na UKIMWI na kuleta mabadiliko chanya. Tuendelee kusimama pamoja, tukipigania haki, usawa, na afya kwa wote. Kwa uwezo wetu tunaweza kushinda changamoto hizi na kujenga Tanzania ambayo inatambua na kuwaheshimu wanawake."

Mratibu wa TACAIDS Dar es Salaam anasema, tume inatambua umuhimu wa ushirikiano kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali, serikali na jamii katika kupambana na UKIMWI na kuwashukuru DWWT kwa jitihada zao za kipekee katika kuboresha afya na ustawi wa wanawake wanaoishi na VVU.

"Ushirikiano wao na TACAIDS umetoa mafanikio makubwa katika kuboresha huduma za afya, elimu, na usaidizi kwa wanawake.Nina furaha zaidi kwa kuwa mratibu wa DWWT pia ni kamishna wa TACAIDS. Na changamoto zilizotajwa nitazifikisha ofisini."

ELIMU
NA FRANK MONYO

# Juhudi za SBL, kuendeleza utalii, kuanza kugusa wasomi elimu ya juu

TANZANIA ni tajiri kwa karibu kila sekta, ukitajwa utalii huko ndiko hazina za taifa zinapojaa na kufurika na ukweli ni kwamba maliasili na utalii hutoa mchango mkubwa wa asilimia 17.5 wa pato la taifa.

Ni eneo linaloiingiza Tanzania asilimia 25 ya fedha za kigeni na pia ni mwajiri wa watu takribani milioni 1.5 wanaofurahia kufanyakazi za aina mbalimbali zitokanazo na sekta hiyo, ni kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mary Masanja, ni Naibu Waziri wa wizara hiyo, anayesema serikali inaelekezwa na ilani ya chama kuhakikisha kuwa sekta ya utalii ifikapo mwaka 2025, inaongeza idadi ya watalii kutoka milioni 1.5 hadi 5,000,000.

Ni wazi kuwa kwa malengo hayo ipo haja ya kuboresha vyuo vya utalii nchini pamoja na kujenga hamasa kwa vijana nchini kukimbilia kusoma vyuoni ili kupata ujuzi hivyo kufanikisha azma ya nchi ya kutembea kifua mbele kwenye utalii, anaeleza Waziri.

Aidha, anakumbusha kuwa utalii unahusisha mambo mengi kama shughuli za kusafiri na kuzuru maeneo na vivutio mbalimbali ili kupata burudani na hata kujifunza.

"Leo Tanzania ina nafasi kubwa ya kuongeza mapato yake na kujinufaisha zaidi ili kukipata kile kilichoko kwenye masoko ya utalii ambacho ni kile utalii unaochataka kutoka kwetu. Tukumbuke tuna kila aina ya vivutio, kuna wanyama, historia kama magofu mbalimbali na michoro ya mapangoni."

Anasema kuna utalii wa maumbile ya asilia kama mabonde na mito, maisha vijijini, chemichemi za maji moto, maporoko na mazingira asilia.

Anakumbusha kuwa ni lazima kuelimisha Watanzania ili kuwa na wataalamu na watu mahiri wenye weledi kuisimamia, kuendeleza na kunufaisha nchi na raia na sekta hiyo.

Maono ya Waziri yanaungwa mkono na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), inayounga mkono juhudi za serikali kuwafunza vijana ili kunufaika na hazina ya taifa inayopatikana kwenye maliasili na utalii.

Meneja Mawasiliano na Mambo Endelevu wa SBL, Rispa Hatibu, anasema kwa kuliona hilo, kampuni itawasaidia wanafunzi katika tasnia ya utalii kupitia mradi wa kujifunza uitwao 'Learning for Life'.



Michoro ya mapangoni iliyoko Kondoa mkoani Dodoma inayovutia watalii. **PICHA: MTANDAO**

> Tangu kuanzishwa kwake mwaka wa 2020, zaidi ya wanafunzi 200 kutoka jamii za wakulima wamenufaika na mpango wa ufadhili wa masomo.

Rispa anasema unawawezesha wanafunzi waonaotoka katika familia zisizojiweza kupata msaada wa kifedha ili kugharamia masomo yao ya elimu ya juu.

Mpango huo ni sehemu ya nguzo ya ushiriki wa SBL katika kusaidia makundi yanayosahaulika kushirikishwa kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, anasema Meneja Mawasiliano na Mambo Endelevu wa SBL.

"Mpango huo unaotarajiwa kuanza mwaka wa fedha wa 2024/25 kwa kampuni ya SBL unaoanza Julai mwaka huu, na hiyo ni nyongeza ya uwekezaji wa kampuni hiyo katika elimu chini ya mpango wa 'Kujifunza kwa Maisha" unaolenga kuboresha uwezo wa kuajiriwa na kujikimu kimaisha," anasema Rispa.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, SBL imekuwa ikiwekeza katika elimu kupitia mpango wa ufadhili wa masomo wa 'Kilimo Viwanda na kwamba chini ya mpango huo ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka jamii za wakulima wanaotaka kusoma kilimo ulitolewa.

"Tangu kuanzishwa kwake mwaka wa 2020, zaidi ya wanafunzi 200 kutoka jamii za wakulima wamenufaika na mpango wa ufadhili wa masomo," anasema.

Rispa anasema kupitia mpango wa SBL wa uanagenzi wa Sayansi, Uhandisi wa Teknolojia na Hisabati (STEM), kampuni hiyo imekuwa ikiajiri vijana wa kike wanaoendelea na masomo ya STEM katika vyuo vikuu ili kuwapa nafasi za mafunzo kazini katika kampuni hiyo.

"Kupitia mpango wa Uanagenzi wa STEM, SBL inatekeleza ajenda yake ya Ujumuishi na Uanuwai, kwa lengo la kuziba pengo la kijinsia katika masomo na taaluma ya STEM," anasema.

Anasema chini ya nguzo endelevu ya SBL, kampuni hiyo imejumuisha elimu kama moja ya vipengele muhimu vinavyojulikana kama 'Learning for Life' ambapo itawekeza kwenye sio tu kusaidia wanafunzi katika masomo ya kilimo na kozi za STEM lakini pia sekta zingine ambazo ni muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ukiwamo utalii.

"SBL, tunasimamia uendelevu, kila kitu tunachofanya kuanzia kwenye biashara hadi uwekezaji wetu katika jamii, tunajitahidi kufanya vitu kwa uendelevu. Ni kwa sababu hii kwamba tumechukua mtazamo sawa linapokuja suala la uwekezaji wetu katika elimu, kwa hivyo neno 'Kujifunza kwa Maisha'.

"Kupitia mpango huu tunajipanga kupanua uwekezaji wetu katika elimu kwa kutoa msaada wetu kwa tasnia ya utalii, kuanzia mwaka wa fedha wa 2024/25," anasema Rispa.

**ZAMU YA UTALII**

Rispa anaongeza kuwa kufuatia mafanikio ya uwekezaji wa miaka minne katika elimu kupitia mpango wa ufadhili wa uanagenzi wa STEM ambao umenufaisha mamia ya wanafunzi na wahitimu, SBL iliona umuhimu wa kutoa msaada wa kifedha kwa wanafunzi katika masomo ya utalii.

"Katika miaka minne iliyopita tumekuwa tukiwasaidia wanafunzi katika kozi za kilimo na sayansi, na mwaka ujao wa fedha, tutapunguza kidogo uwekezaji wetu katika programu kama kilimo viwanda, ingawa tutaendelea kuunga mkono juhudi katika sekta hizi mbili, tulitaka kuongeza msaada katika sekta ya utalii pia, kwa kuzingatia kwamba hii ni moja ya sekta muhimu zinazochangia kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi yetu na uboreshaji wa maisha,"anasema Rispa.

Anabainisha kuwa, mwaka ujao wa fedha unapokaribia, SBL itatoa maelezo zaidi kuhusu mpango wake wa 'Kujifunza kwa Maisha' katika tasnia ya utalii ikiwa ni pamoja na vipimo na vigezo vya kunufaika na programu hiyo, idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kufaidika pamoja na vyuo na wadau wengine wakuu ambao SBL itashirikiana nao kutekeleza mpango huo kwa mafanikio.

Pamoja na kuwekeza kwenye elimu katika mwaka ujao wa fedha, SBL itaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya jamii akitaja mpango wa Society 2030: Spirit of Progress.

"Hii itahusisha kuwekeza katika miradi ya maji kupitia nguzo yake ya 'maji ya uhai' pamoja na kwenye ajenda ya uendelevu."Anaongeza.



## TFRA yaboresha mfumo utoaji mbolea za ruzuku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imeboresha mfumo wa utoaji mbolea za ruzuku ambao hivi sasa utakuwa ukionyesha aina ya mazao mkulima anayolima ili aweze kuhudumiwa mbolea stahiki inayoendana na aina ya mazao.

Mfumo wa awali ulikuwa ukiruhusu mkulima kupata mifuko mitatu kwa ekari moja, bila kujali aina ya mazao yanayolimwa na wakulima na kusababisha changamoto kwa wakulima kutokupata mbolea inayokidhi mahitaji.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku ya TFRA, Louis Kasera, wakati akizungumza na kituo kimoja cha redio jijini hapa katika mahojiano ya moja kwa moja na maofisa ugani kutoka wilaya za mkoani hapa kwenye mkutano wao uliofanyika jana.

Mwenyekiti huyo aliwataka wakulima kuendelea kujisajili ili waweze kuingia kwenye mfumo ambao utawawezesha kupata mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali.

"Naomba wakulima ambao hawajajisajili kwenye mfumo waendelee kujisajili, hivi sasa mfumo umeboreshwa ambao utamwezesha mkulima kupata mbolea stahiki," alisema Kasera.

Alifafanua kuwa hiyo itawasaidia wakulima kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi ikiwamo kuleta matokeo chanya kwa taifa.

Kaimu Meneja wa Kanda, Joshua Ng'ondya, alisema wakulima wanapopata mbolea ya ruzuku wanapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku wanayopewa na wataalamu ili kuongeza tija kwenye kilimo wanachofanya.

"Si kweli kuwa mbolea inaharibu udongo isipokuwa mkulima anapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija kwenye kilimo chao," alisema Ng'ondya. Alisema pia mbolea aliharibu udongo isipokuwa matumizi yasiyo sahihi ya mbolea ndiyo yanayosababisha tija isipatikane, mkulima anapaswa azingatie matumizi sahihi ya mbolea.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo Mkoa wa Dodoma, Bernard Abraham, alipongeza uamuzi wa TFRA wa kukutana na wasimamizi wa kilimo katika ngazi ya mkoa na wilaya na kuweka mikakati ya pamoja ya kuhakikisha azma ya kuwahudumia wakulima imefikiwa.

"Mwaka huu TFRA wamefanya vizuri sana wameamua kukutana nasi na wamekuja kwa wakati na wameheshimu sana uwapo wetu kwa kutambua kuwa sisi ndio tupo karibu na wakulima," alisisitiza.

Alisema mkoa wake umejipanga kuhakikisha wanahuisha taarifa za wakulima na kusajili wapya mapema ili kuwawezesha kupata bidhaa hiyo ifikapo Julai, 2023 ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa mbolea baada ya msimu kupita.

# Ataka fedha za posho zitumike kununua taulo za kike

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, ameyataka mashirika yanayojihusisha na masuala ya hedhi salama nchini kupunguza matumizi ya fedha kwa ajili ya malipo ya posho za vikao ili kiasi hicho kitumike kununua taulo za kike kwa ajili ya kuzisambaza kwenye shule.

Dk. Mollel alisema hayo juzi alipokuwa akihutubia kwenye maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani iliyofanyika kitaifa jijini hapa.

Alisema wadau wa masuala ya hedhi salama badala ya kuendelea kueleza kero zilizopo kwa wasichana na wanawake nchini, wanapaswa kutafuta suluhu.

"Badala ya kuendelea kupiga kelele kuhusu suala la changamoto wanazokumbana nazo wasichana na wanawake nchini mnapaswa kufanya kitu ambacho kitatoa majibu ikiwamo kubana matumizi katika malipo ya posho zenu za vikao ili fedha hizo zitumike kwenye ununuzi wa pedi na mzigawe katika mashule nchini," alisema Dk. Mollel.

Kadhalika, alisema wadau hawapaswi kuendelea kuzungumza kuhusu kero mbalimbali zilizopo bila ya kuwa na mipango ya kuhakikisha taulo za kike zinapatika katika maeneo ya shule ili wanafunzi kushiriki masomo bila bugudha.

"Hatupaswi kuendelea kuzisema changamoto hizi bila kuweka mipango ya kuwa na uhakika wa kupata pedi angalau milioni tano katika kipindi kama hichi mwakani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewasaidia sana watoto wetu," alisema.

Dk. Mollel, alisema anatamani maadhimisho ya mwaka ujao ya siku ya hedhi salama duniani yafanyike vijiji kwa ajili ya kugawa taulo za kike kwa wanafunzi tofauti na ilivyokuwa mwaka huu.

"Mimi nataka mwakani tusiwe na maadhimisho ya ukumbini mjini kama mwaka huu nataka tutoke kwenda kugawa pedi katika shule mbalimbali maeneo ya vijijini tofauti na ambavyo tunafanya leo kueleza changamoto bila kuchukua hatua," alisema.

Vile vile, alitoa maelekezo kwa TAMISEMI kuhakikisha ujenzi wa vyoo unazingatia vyumba kwa ajili ya wasichana kujihifadhia wanapokuwa kwenye kipindi chao cha hedhi.

"Ujenzi wa vyoo vyetu vya shule lazima viendelee kuzingatia vyumba kwa ajili ya kujisitiri watoto wa kike, lakini tuweke bajeti kwa ajili ya mashine za kuuzia taulo za kike katika kila shule," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akitoa maelezo kwa wasimamizi wa miradi ya ujenzi wa madarasa kuhakikisha unakamilika kwa wakati na ubora unaokubalika. Senyamule alikagua Shule ya Msingi Kisasa na Swaswa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadhamiria kuanzisha benki yao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania (FEMATA), linatarajia kuanzisha benki yao ambayo itatumika kuwakopesha wachimbaji ili kuinua sekta hiyo muhimu kiuchumi nchini.

Rais wa FEMATA, John Bina, alisema hayo jana kwenye kikao cha Kamati Tendaji ya shirikisho hilo kilichoitishwa ili kukamilisha mchakato wa kuandika Katiba mpya ambayo itaendana na wakati wa sasa.

Bina alisema wataanzisha benki hiyo ili kuwasaidia wachimbaji kukopeshwa fedha za mitaji ya kuendesha shughuli za uchimbaji baada ya kuwapo changamoto za kukopeshwa fedha na benki za hapa nchini.

"Wachimbaji tumekuwa na changamoto kubwa tunatumia zana duni kufanyia kazi zetu kutokana na kuwa na mitaji midogo na kibaya zaidi hata tukienda katika benki zilizopo kuomba mkopo hatukopeshwi," alisema.

Aidha, alisema ili shirikisho hilo lililoanzishwa tangu mwaka 1986 wamekubaliana kuiboresha katiba yao iliyopo iendane na wakati FEMATA iendelee kuwa imara.

Bina alitumia nafasi hiyo kuwahamasisha wananchi wa Mkoa wa Singida kuchangamkia fursa ya uchimbaji wa madini mengi ya aina mbalimbali yaliyopo mkoani hapa.

"Singida ina akiba ya madini ya kutosha, lakini changamoto iliyopo ni ya rasilimali watu mimi kwetu ni hapa Singida lazima niwaambie acheni uzembe fanyeni kazi wenzetu Wasukuma ndio wanaofanya kazi ya uchimbaji wa madini katika migodi iliyopo," alisema. Aidha, Bina alizungumzia tozo wanazotozwa wachimbaji kwenye halmashauri za wilaya wanapotunga sheria wawe wanawashirikisha viongozi wa FEMATA kwa kuwa zimekuwa nyingi na kuwa kero kwao.

Alisema changamoto nyingine iliyopo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuja na mfumo wa kuwatoza kodi kwa asilimia mbili na kwamba hawakatai kulipa kodi kwa kuwa ndio msingi wa maendeleo na kuiomba mamlaka hiyo iangalie namna ya kuiondoa kodi hiyo ambayo imekuwa kero.

Bina aliomba TRA wakae pamoja na wachimbaji kujadili kodi hiyo iliyoanza kutozwa ili kuwe na namna bora ya kuliweka sawa jambo hilo bila kuumiza upande wowote.

Ofisa Mkazi wa Madini Mkoa wa Singida, Chone Malembo, aliomba shirikisho hilo kufungua milango ya kuwaita wachimbaji wengine kutoka mikoa mingine kuja kuwekeza mkoani Singida.

# Samia achangia milioni 2/- ujenzi wa kanisa

**Na Nebart Msokwa,**
MUFINDI

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa msaada wa Sh. 2,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kanisa la Tanzania Evangelistic Assemblies of God (EAGT) Mafinga mkoani Iringa.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alikabidhi msaada huo jana kwa niaba ya Rais aliposhiriki ibada kwenye kanisa hilo na kuwataka waumini wa kanisa hilo kuendelea kuliombea taifa. Alishiriki ibada hiyo akiwa katika mwendelezo wa ziara yake ya siku sita mkoani humo yenye lengo la kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero za wananchi pamoja na kukagua uhai wa chama hicho.

Chongolo aliwaomba wananchi hao pia kumwombea Rais Samia pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali ili waendelee kuliongoza vyema taifa na liendelee kuwa na amani.

"Nilipomwambia rais kwamba leo nataka kushiriki ibada kwenye kanisa hili, ameniagiza niwapatie fedha hizi kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kanisa lenu ambalo mnaendelea kujenga, lakini ameomba niwaambie kwamba anawapenda na anaomba mwendelee kumwombea," alisema Chongolo.

Mchungaji wa kanisa hilo, Dk. Wallace Howa Howa, alimshukuru Rais Samia kwa msaada huo na kuwa fedha walizopewa zitasaidia kukamilisha ujenzi wa kanisa hilo ambalo wamelijenga kwa awamu tofauti.

Alisema mpaka sasa ujenzi umefikia hatua ya ukamilishaji na walikuwa wanahangaika namna ya kupata fedha ya kukamilisha kwa kuanza kuchangishana ili kupata fedha hizo.

Alisema baada ya msaada huo wa Rais Samia, watalikamilisha haraka kanisa hilo tofauti kama wangetumia utaratibu wa kuchangishana kutokana na hali ya uchumi wa waumini sio nzuri.

"Tunaomba utufikishie salamu zetu kwa rais wetu, upendo huu aliotuonyesha tunahakikisha kwamba tunaendelea kumpenda na kumuombea, hatuna kitu cha kumpatia lakini tutaendelea kumwombea," alisema Mchungaji Howa Howa.

Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo anaendelea na ziara katika Mkoa wa Iringa akiwa ameambatana na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema, pamoja na Katibu wa Oganizesheni, Issa Haji Ussi maarufu kwa jina la 'Gavu'.



Katibu Tawala Mkoa wa Mara, Msalika Makungu (kulia), akikata utepe kuzindua huduma ya usafiri wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga ili kuokoa vifo vya mama na motto, hafla iliyofanyika Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kwangwa, (wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa Dijitali na Huduma za Ziada wa Vodacom Tanzania PLC, Mhandisi Nguvu Kamando.
Zaidi ya kinamama 21,800 na watoto wachanga wamesafirishwa kupitia mfumo huu, ambapo takribani maisha 806 yameokolewa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WaterAid yaona changamoto wasichana wawapo kwenye hedhi

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Shirika la WaterAid Tanzania, Anna Mzinga, amesema bado kuna changamoto ya wasichana kukosa vipindi vya shule kutokana na upungufu wa vyumba maalum vya kujistiri wakati wanapoingia kwenye hedhi.

Mzinga aliyasema hayo juzi mkoani Tanga wakati akikabidhi msaada katika Shule ya Sekondari ya Misima iliyopo Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, alikabidhi cherehani moja kwa ajili ya wanafunzi kujishonea pedi za kitambaa, vifaa 40 vya kushonea pedi na katoni 55 za pedi za kutumika katika kipindi cha mvua endapo pedi za kufua zitashindwa kukauka.

Vifaa vingine ni vya michezo seti tatu, mabango 20 kwa ajili ya kujifunza masuala ya usafi na televisheni kwa ajili ya kujifunza tabia siha na usafi kwa ujumla.

"Licha ya jitihada za dhati zimefanywa na serikali na wadau ila bado inaripotiwa asilimia 34 ya wasichana hukosa vipindi shule kutokana na upungufu wa vyumba maalumu vya kujisitiri wakati wa hedhi huku asilimia 26 kutokana na ukosefu wa maji na vyoo safi katika shule," alisema Mzinga.

Alisema kaulimbiu ya kitaifa ya siku ya hedhi inayosema "Hedhi ni tunu na msingi wa afya kwa wasichana na wanawake, tuiwezeshe," ni muhimu kuendelea kuweka mkazo katika masuala ya hedhi iliyo salama kwa wasichana na kinamama kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo."

Aidha, alisema katika kuadhimisha siku ya hedhi kila Mei 28, duniani shirika lake liliungana na wanafunzi na walimu katika shule hiyo kuwakabidhi mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji na mafunzo ya tabia siha uliofadhiliwa na Shirika la Hilton Global Foundation na WaterAid, ili kupunguza makali ya ukosefu wa maji katika shule hiyo hasa kwa watoto wa kike wanapokua katika kipindi cha hedhi.

"Tumefanikisha ukarabati wa miundombinu kadhaa ya mfumo wa maji, matengi ya kuhifadhia maji, kuweka miundombinu ya choo rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kutoa elimu kuhusu usafi kwa wasichana na wavulana katika hatua za makuzi yao binafsi, hii ilijumuisha mafunzo maalumu ya namna ya kujitengezea taulo za kike za kujisitiri wakati wa hedhi, kujilinda na adha mbalimbali wanapokua katika kipindi cha hedhi," alisema Mzinga.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Upendo Magashi, alisema miundombinu iliyowekwa inahitajika kutunzwa ili iendelee kutoa huduma kwa kipindi kirefu na wanafunzi kunufaika.

WaterAid ni shirika la kimataifa lenye dira ya kuhakikisha watu wote ulimwenguni wanapata maji ya uhakika, vyoo bora na huduma za usafi zilizoboreshwa ifikapo mwaka 2030.

Shirika hilo linafanya kazi katika nchi 28, ambapo nchi 18 zipo barani Afrika. Nchini Tanzania, Shirika la WaterAid lilianza kazi 1983 na kufanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji, vyoo na usafi binafsi katika zaidi ya mikoa 11.

Aidha, shirika limeshirikiana na serikali na wadau wengine wa maendeleo na kuwafikia wananchi zaidi ya milioni nane wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa miji na vijijini.

# 'Smart meter' za LUKU kuanza karibuni

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema utaratibu wa kutumia mita za kuweka umeme kama ilivyo kwa ving'amuzi (smart meter), unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Kuanza kutumia kwa mita hizo kutasaidia kuondoa usumbufu kwa wateja wa kuingiza namba kwenye mita za umeme kama inavyotumika sasa kwa mita za zamani.

Mita za sasa za umeme, mteja hulazimka kuingiza namba ndipo umeme uwake, lakini zitakapoanza kutumika za kisasa, umeme utakuwa unawaka moja kwa moja baada ya kununuliwa kama ilivyo kwenye king'amuzi.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Maharahe Chande, alisema maandalizi ya kufikia katika hatua hiyo ni mazuri.

Alisema kupitia mfumo huo, umeme utawaka mara mteja anaponunua.

"Mfumo huu utakuwa kama ilivyo kwa king'amuzi, kwamba unaponunua tu umeme unawaka sio mpaka uingize token zake," alisema Chande.

"Ili tufikie katika hatua hii ni lazima tuwe na smart meters na hili nalo tunakamilisha hivi karibuni na halitachelewa kwa sababu kimekuwa ni kilio cha muda mrefu wakitaka kuwapo kwa mfumo ambao utawawezesha umeme kuingia bila kuingiza kwenye mita."

Katika Mkutano huo, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Kuhusu kama Tanesco ina mpango wa kushusha bei ya kuunganisha umeme baada ya kuanza uzalishaji wa nishati hiyo katika Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), Chande alisema hadhani kama sio rahisi kushusha gharama hizo baada ya mradi huo kuanza uzalishaji.

"Huwezi kushusha kuunganisha umeme baada ya kuanza kuzalisha JNHPP wakati hata miundombinu inayojengwa kwa kutumia mapato yanayotokana na uuzwaji wa umeme haijakamilika," alijibu Chande.

Kuhusu vyura wa Kihansi kurejeshwa nchini, swali liliulizwa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, Chande alisema vyura hao wanaohifadhiwa nchini Marekani wataanza kurejeshwa nchini Julai, mwaka huu.

Alisema wakati vyura hao wanapelekwa Marekani, Tanzania haikuwa na maabara na kwamba hata mwaka 2021 ambao walitakiwa kuwarejesha walishindwa kufanya hivyo kwa sababu ya Uviko-19.

Alisema vyura waliopelekwa ni 500, lakini wamezaliana na kuongezeka zaidi na kwamba katika kipindi chote walichohifadhiwa huko nchi imepata faida.



## Nyumba za maendeleo zaanza kufanyiwa ukarabati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba la Zanzibar, limesema limejipanga kuhakikisha nyumba za maendeleo zinafanyiwa ukarabati mkubwa ambazo baadhi yake zipo katika hali mbaya ya uchakavu na kutishia maisha ya wakazi wake.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Ardhi, Maendeleo ya Makazi, Juma Makungu, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, Salim Nassor Jazira, aliyetaka kujua shirika lini litazifanyiya ukarabati nyumba za maendeleo ambazo baadhi yake zipo katika hali mbaya.

Makungu alisema serikali katika mwaka wa fedha 2022-2023 imepanga kutekeleza mradi wa ukarabati wa nyumba za maendeleo kwa kutenga bajeti ya Sh. bilioni 16.

Alisema kutokana na ukosefu wa bajeti ya kutosha fedha hizo hazikupatikana na shirika lilishindwa kutekeleza dhamira yake.

Alisema, kwa kutumia fedha za makusanyo ya kodi za wapangaji wa nyumba za maendeleo, shirika lilifanikiwa kufanya ukarabati wa jengo la flati namba 10 liliopo Michenzani katika eneo la Kisonge na kurudisha haiba yake katika eneo hilo.

Aidha, alisema Shirika la Nyumba linafahamu uchakavu wa nyumba za maendeleo zilizopo katika kisiwa cha Pemba ambazo zipo katika hali mbaya huku nyingine zikikimbiwa na wapangaji wake.

Alizitaja nyumba hizo ikiwamo Mtemani, Chakechake, Wete pamoja na Kengeja ambazo shirika limelazimika kuwahamisha wapangaji wake.

"Mheshimiwa Naibu Spika napenda nikiri kwamba nyumba za maendeleo ziliopo Pemba zipo katika hali mbaya ya uchakavu wake huku nyingine zikipasuka kuta zake na kulazimika wapangaji wake kuhamishwa ikiwamo Kengeja, Pemba," alisema. Makungu aliwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwahamasisha wapangaji katika nyumba za maendeleo kuhakikisha wanalipa kodi ya nyumba na fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ukarabati.

"Nawaomba wapangaji wa nyumba za maendeleo kuhakikisha wanaharakisha kulipa kodi ya mwezi kwa ajili ya kutumia fedha hizo kufanya matengenezo ya nyumba," alisema.

# ACT yahoji ripoti CAG kuwasilishwa kimya kimya

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema serikali inapaswa kueleza kwa nini ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar (CAG) ya mwaka 2022 imewasilishwa kimya kimya bila ya kutangazwa hadharani kinyume na misingi ya utawala bora.

Hayo yamesemwa na mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho katika viwanja vya Garagara Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, uliojadili mwelekeo wa hali ya kisiasa na kiuchumi Zanzibar.

Alisema serikali ya awamu ya nane tangu kuingia madarakani imekuwa ikiweka wazi ripoti ya CAG, lakini inaonekana zililenga serikali ya awamu ya saba na ndio maana ripoti ya mwisho haijawekwa hadharani kwa vile inagusa mambo yaliofanyika chini ya serikali hiyo na kuwasilishwa kimya kimya.

Alisema Zanzibar kumeibuka tatizo la miradi ya ujenzi kutofanyika kwa uwazi pamoja na ukodishwaji wa taasisi za huduma kama ilivyofanyika katika Bandari ya Malindi Unguja kupewa mwekezaji kuendesha.

Alisema serikali imekuwa ikijivunia kuongeza ukusanyaji wa mapato kupitia huduma za bandari na kununua vifaa vya kisasa vya uchukuzi na upakizi yenye thamani ya mabilioni ya fedha na kuhoji kwanini apewe mwekezaji kutoka nje ya nchi.

Kadhalika, alisema uwekezaji uliofanyika katika huduma za bandari haukufanyika kwa uwazi na serikali inapaswa kueleza ilitangaza lini zabuni na serikali itanufaika vipi katika uwekezaji huo ili wananchi kufahamu kwa sababu eneo hilo ni nyeti katika uchumi wa Zanzibar.

"Tunawasiwasi wa watu kupoteza ajira kama ilivyotokea katika huduma za uwanja wa ndege jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume baada ya kupewa kampuni ya Dnata kutoka nchini Dubai.

"Zanzibar imegeuzwa shamba la bibi Rais Samia amesaidia sana Zanzibar kupitia fedha za UVIKO-19 miradi ya maendeleo, lakini fedha hizo zimevurugwa na kutotumika ipasavyo," alisema Jussa.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisema serikali sio mali ya mtu na inapaswa shughuli zote za serikali kufanyika kwa uwazi kwa maslahi ya nchi na wananchi wake.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema kumbukumbu zinaonesha kwamba Zanzibar imekuwa na taasisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali miaka 10 baada ya mapinduzi na lengo lilikuwa kutambua matumizi ya fedha za umma ili wananchi wafahamu matumizi yake.

Alisema Zanzibar haiwezi kupiga hatua ya maendeleo bila ya kuwa na mamlaka kamili ya mfumo wa Muungano na kuwataka wananchi wake na viongozi kutumia fursa ya mchakato wa katibu ulioamuliwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano.

Alitahadharisha kuwa Rais Samia hatopendelea upande wowote wa Muungano bali hoja za wananchi na mshikamano wa viongozi ndio utakaosaidia kupata katiba bora yenye kuzingatia mambo ya msingi yanayohitaji Zanzibar katika mfumo wa muungano.

"Tunatakiwa kukaa katikati kutetea maslahi ya Zanzibar, tusiwape nafasi chawa kwa sababu Zanzibar inahitaji kutetewa na Wazanzibari wenyewe na mama Samia ni mtu anayelinda maslahi ya pande zote, tusimtegemee yeye kwa sababu yeye ni dereva, lakini anaendesha gari sio lake...tukikosa hapa tutakua tumetolewa vikoa," alisema Othman.

Aidha, alisema licha ya kuwapo kwa serikali ya umoja wa kitaifa bado kuna vitendo vya kiubaguzi katika suala la ajira na upatikanaji wa vitambulisho vya Mzazibari mkaazi.

Naye mwanasiasa maarufu na mshauri wa chama hicho Mansour Yussuf Himid, alisema inashangaza utaratibu unaotumiwa na serikali wa kuvunja barabara ambazo bado nzima na kuacha kujenga barabara ambazo zipo katika hali mbaya.

Alisema barabara iliyovunjwa ya kutoka Uwanja wa Ndege hadi Mnazi Mmoja ilitumia gharama kubwa kutengenezwa ikiwamo kuwekwa mitaro ya maji ambayo ilitumia gharama kubwa ya ujenzi wake mwaka 2020.

Alisema wakati umefika serikali kuwa na vipaumbele vya msingi ikiwamo kuimarisha huduma bora za matibabu kuondoa tatizo la umaskini ili kufufua matumaini mapya ya wananchi ya kuwapatia huduma bora.



Baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa, wakuu wa wilaya na mikoa, makamanda wa polisi wa mikoa na wilaya walioshiriki mafunzo kuhusu uzingatiaji wa masuala ya watu wenye ulemavu yaliofanyika Mjini Zanzibar wakimsikiliza Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, aliyefungua mafunzo hayo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali yaeleza sababu mamba wa Bara kuonekana Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR ina historia ya kujitokeza mamba kutoka Tanzania Bara hasa katika kipindi cha mvua kubwa wakati mito inaposhindwa kukabiliana na maji yanayotokana na mafuriko.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleman Makame, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi huko Chukwani, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Hamad, aliyetaka kujua kauli ya serikali baada ya kuonekana kwa mamba katika bahari ya Kiwengwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja hivi karibuni.

Alisema baadhi ya mito ya Tanzania Bara kama Pangani, Saadani, Ruvu pamoja na Wami humwaga maji hayo ya mafuriko katika Bahari ya Hindi na upo uwezekano mkubwa wa wanyama hao kutumbukia na kukokotwa na maji hadi baharini na hatimaye kufika Zanzibar.

"Kwa mfano mwaka 1917, mamba alionekana bahari ya Chwaka, 1939 mamba alionekana bahari ya Mtende, 1945 mamba alionekana bahari ya Nungwi, 1952 mamba walionekana bahari ya Matemwe na Muwanda, 1962 mamba alionekana bahari ya Makunduchi, hivyo kwa kuwa wanyama hao wana uwezo wa kuishi katika maji ya bahari ingawa kwa kipindi kifupi ni wazi kuwa wanasafirishwa na maji kutoka mikoa ya Tanzania Bara hadi visiwani kwetu," alisema.

Alisema, serikali ina taarifa za kutosha na Aprili 13, mwaka huu, huko Kiwengwa Kairo, alionekana mnyama aina ya mamba akiogelea katika bahari na kukamatwa na wananchi kwa kushirikiana na watendaji wa serikali.

Kadhalika, wizara yake ilipokea taarifa kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhusu kuonekana kwa mamba huyo katika bahari ya Kiwengwa Kairo ilishirikiana na Wizara ya Kilimo kupeleka watendaji wake ambao walishirikiana na wavuvi wa eneo hilo na kufanikiwa kumdhibiti mamba huyo bila ya kumuathiri na kutomdhuru mtu yeyote.

"Kwa sasa mamba huyo anahifadhiwa katika zizi maalum la Idara ya Misitu liliopo Dole kwa ajili ya uangalizi zaidi," alisema.

Hata hivyo, alisema kibaiolojia mamba wa maji baridi ambao wanapatikana Tanzania wanaweza pia kuishi ndani ya maji ya bahari kwa kuwa ndani ya mwili wa mnyama huyo zipo tezi (glands) ambazo zina uwezesha mwili wake kutoa nje kiwango cha chumvi iliozidi kwa kipindi kifupi.

Alisema kimaumbile mamba maji baridi hawezi kuishi katika maji bahari kwa kipindi kirefu hivyo endapo ataendelea kuishi ndani ya maji chumvi kwa kipindi kirefu kiwango cha chumvi kitaongezeka katika mwili wake na kuathiri chembe hai na kupelekea kifo kwa mnyama huyo.

Masoud alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa nyakati tofauti zilitoa tamko juu ya tukio hilo na kuwanasihi wananchi kuwa watulivu kwa sababu matukio hayo ni nadra hutokea hivyo wananchi waondoe wasiwasi na waendelee kufanya kazi zao za kujipatia kipato.

"Tunawaomba wananchi wasisite kutoa taarifa na kuwa tayari kushirikiana na serikali endapo watabaini tukio jingine la kuonekana kwa mamba katika eneo lote la Zanzibar," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**LEOCADIA BONIPHAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0784-0063** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AIR WING SEKONDARI** mwaka **1999**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **STK/RB/1779/04**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**HILDA DANIEL GALATON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5022-0007** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LONAT SEKONDARI** mwaka **2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/224708/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KHAYRA NASSOR MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2626-0024** kilichotolewa na **CHARLOTTE SEKONDARI** mwaka 2013. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0310/0505** kilichotolewa na **FOREST HILL SEKONDARI** mwaka 2016. Cheti cha Chuo Diploma kilichotolewa na TUMAINI UNIVERSITY mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **MOR/MOR/RB/174300/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**REHEMA PHILBERT MBEPERA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P-09380381 kilichotolewa na **MBEZI BEACH SEKONDARI** mwaka 2017. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba P-04380127 kilichotolewa na **MASJID QUBAH MUSLIM SEMINARY CENTRE** mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/MAG/RB/104449/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRUNO DIDAS SHAO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 424 ANN TOYOTA RAV 4** yenye Chassis **No. SXA110046418.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/180424/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSA DAVID MWANKINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 703 DDZ** Toyota Coaster. Engine No. **1HZEAA8930** chassis No. **HZB500008930.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/B/26206/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HANNAH SEIF MSAKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 722 BCU TOYOTA FAN CARGO.** Chassis **NCP2001128643. ENGINE 2NZ1459622.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/182350/2023.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(DISTRICT REGISTRY OF MOROGORO)**
**AT MOROGORO**
**LAND APPEAL NO. 8 OF 2023**
***(Arising from the Land Application No. 30 of 2018 From Morogoro District Land and the Housing Tribunal at Morogoro)***
**JAPHET MBOGO...............APPELLANT**
**VERSUS**
**JUMA A. TEMBO..................1ST RESPONDENT**
**DANIEL MCHOME ..........2ND RESPONDENT**

### NOTICE OF HEARING

**TO DANIEL MCHOME**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on **5th day of June 2023 at 09:00 AM** at the High Court of Morogoro.
Your required to appear in person or through your Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and your directed to produce on that day all documents which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed to hear the Civil Case and pronounce judgment in your absence.
**GIVEN** under my **HAND AND SEAL** of the court this **25th day of May 2023**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT
MOROGORO

**AMANDI E.A LIMITED**
**CHETI CHA USAJILI NAMBA 97727**
**SHERIA YA MAKAMPUNI, 2002**
**(KIFUNGU 334 (1))**
**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha **AMANDI E.A LIMITED** (Kampuni), yenye usajili namba 97727, kilichofanyika tarehe 15 Mei 2023 azimio maalumu lilipitishwa.:

- Kufuatana na kifungu 331(1)(b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa Kampuni ifutwe kwa hiari na
- Wanahisa wamemteua J**OHNPAUL THADEI MWAKILASA** wa Mikumi House, 368 Msasani Road, Oysterbay, S.L.P 9673, Dar es salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa Kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupokea madai yao kwa usaliti ndani ya siku thelathini (30). maombi yote yatakayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

JOHNPAUL THADEI MWAKILASA
MFILISI wa AMANDI E.A LIMITED

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.69/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU LEVINA LAURENT TARIMO WA DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ESTHER JOSEPH SWAI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 09 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 25 Mwezi 05 Mwaka 2023

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mkataba usitishaji mapigano wakiukwa Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MILIO ya risasi imesikika katika mji mkuu wa Sudan, Khartoum na kuashiria ukiukaji wa mkataba wa usitishaji mapigano wakati Marekani na Saudi Arabia zikisema mapigano hayo yanazuia usafirishaji wa misaada ya dharura.

Nchi hizo mbili ambazo ni wapatanishi katika mzozo wa Sudan zimetoa wito kwa mkataba huo wa kusitisha mapigano kurefushwa.

Wakazi mjini Khartoum wameliambia shirika la habari la AFP kuwa, wamesikia milio ya risasi kusini mwa mji mkuu huo katika siku ya sita ya mkataba wa wiki moja wa usitishaji mapigano.

Kwa mujibu wa Marekani na Saudi Arabia, mkataba huo ambao unalenga kuruhusu ufikiaji wa misaada ya kibinadamu kwa raia umekiukwa na pande mbili za jeshi zinazohasimiana na kuzuia kwa kiasi kikubwa, malengo ya kusafirisha misaada.

Takwimu za shirika la utafiti wa mizozo la (ACLED) zinaonyesha kuwa zaidi ya watu 1,800 wameuawa katika wiki sita za mapigano.

Mapigano hayo yanayoendelea ni kati ya jeshi la Sudan linaloongozwa na mkuu wa jeshi Jenerali Abdel al-Burhan na makamu wake wa zamani, Mohamed Dagalo, ambaye anaongoza kikosi cha msaada wa dharura RSF.

Taarifa ya pamoja ya Marekani na Saudi Arabia imesema pande zote mbili zimevuruga juhudi za kusafirisha misaada ya kibinadamu, ikiwamo kuwatuma wapiganaji wake karibu na hospitali katika eneo linalodhibitiwa na RSF huku watu waliovalia sare za kijeshi wakidaiwa kuiba vifaa vya matibabu.

UN ilisema kikosi cha RSF kimechukua udhibiti wa nyumba za raia, biashara za watu binafsi na majengo ya umma ambayo baadhi yake yameporwa. **DW**



Jenerali Abdel al-Burhan



Mohamed Dagalo

# Sheria kupinga mapenzi jinsia moja yapitishwa rasmi Uganda

**KAMPALA,** Uganda

SPIKA wa Bunge la Uganda, Anita Among, ametangaza kuwa Rais wa taifa hilo, Yoweri Museveni, ametia saini muswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja kuwa sheria.

Spika Anita, aliyabainisha hayo jana kupitia taarifa aliyoituma kwenye mtandao wa Twitter, akieleza kuwa Rais Museveni, ametekeleza majukumu yake ya kikatiba kama ilivyoainishwa na ibara ya 91 (3) (a) ya katiba ya kuidhinisha sheria ya kupinga mapenzi ya jinsia moja.

**Kwa Mungu na nchi yangu, daima tutasimamia na kuendeleza maslahi ya watu wa Uganda.**

"Kama Bunge la Uganda, tumejibu kilio cha wananchi wetu. Tumetunga sheria ili kulinda utakatifu wa familia kulingana na Kifungu cha 31 cha Katiba ya Uganda," alisema Anita.

"Tumesimama kidete kutetea utamaduni wetu na matarajio ya watu wetu kulingana na malengo ya ibara ya 19 na 24 ya malengo ya kitaifa na kanuni za maagizo ya sera ya serikali. Namshukuru rais, kwa hatua yake thabiti kwa maslahi ya Uganda," alisema Anita.

Aliongeza kuwa "kwa Mungu na nchi yangu, daima tutasimamia na kuendeleza maslahi ya watu wa Uganda".

Pia aliwashukuru wananchi wa Uganda kwa maombi na kutia moyo walipotekeleza wajibu wao kwa mujibu wa ibara ya kwanza na 79 ya katiba ya nchi hiyo.

Aidha, aliwataka watekelezaji kutekeleza mamlaka waliyopewa kisheria ya kupinga mapenzi ya jinsia moja.

Hata hivyo, ikulu ya Uganda katika ukurasa wake wa Twitter imetuma picha ya Museveni kuthibitisha kuwa rais huyo ametia saini muswada huo. **BBC**



Raia wa Sudan wakikimbilia katika kambi ya wakimbizi ya Borota iliyoko Chad, karibu na mpaka wa Jimbo la Darfur baada ya mkataba wa usitishaji mapigano kutozingatiwa. **PICHA: MTANDAO**

# Erdogan ashinda tena uchaguzi Uturuki

**ANKARA,** Uturuki

RAIS wa Uturuki, Recep Erdogan, ameshinda tena katika kinyang'anyiro cha urais ikiwa ni jitihada za kuongeza muda wa utawala wake wa miongo miwili itakayompa dhamana ya kutawala taifa hilo hadi 2028.

Wananchi nchini Uturuki walilazimika kufanya uchaguzi wa rais kwa mara ya pili baada ya awamu ya kwanza kugubikwa na madai ya kutokuwa na usawa na baada ya kufanikiwa kushinda Rais Erdogan jana alitoa wito kwa wananchi juu ya kudumisha mshikamano wa kitaifa.

Ilielezwa kuwa kiongozi huyo amefanikiwa kuruka kiunzi cha mzozo mbaya zaidi wa kiuchumi nchini humo na pia kuhimili ushindani mkali kutoka kwa muungano imara wa upinzani kuwahi kukikabili chama chake cha Kiislamu.

Maelfu ya watu walijitokeza barabarani kwa shangwe na nderemo wakati kiongozi muhimu zaidi katika historia ya kisiasa ya Uturuki alipowaongoza wafuasi wake kwa nyimbo za ushindi nje ya ikulu ya rais mjini Ankara.

Matokeo yaliyokaribia kukamilika yameonyesha Erdogan amemshinda mpinzani wake Kemal Kilicdaroglu kwa zaidi ya asilimia nne ya kura zilizohesabiwa.

Kwa mujibu wa baraza kuu la uchaguzi, Erdogan amejizolea asilimia 52.14 ya kura huku mpinzani wake akipata asilimia 47.86.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani, Joe Biden, amempongeza Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan kufuatia ushindi wake katika duru ya pili ya uchaguzi.

Kupitia mtandao wake wa Twitter, Biden ameandika kuwa anatarajia kuendelea kufanya kazi kwa pamoja kama washirika wa muungano wa kijeshi wa NATO katika masuala muhimu kati ya Ankara na Washington na ushirika katika kukabiliana na changamoto za kimataifa. **DW**

# Uwakilishi wa Russia wazuru Kenya

**NAIROBI,** Kenya

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, amewasili jijini Nairobi, nchini Kenya katika ziara ambayo haikutangazwa.

Ukurasa wa Twitter wa Ubalozi wa Russia nchini Kenya, uliandika jana kuwa itakuwa ni wiki ya mafanikio kati ya Kenya na Russia.

Ilielezwa kuwa ziara hiyo ya waziri wa Russia imekuja baada ya mwenzake wa Ukraine, Dmytro Kuleba, kufanya ziara barani Afrika.

Pia inatarajiwa kuwa huenda kiongozi huyo akakutana na Rais wa Kenya William Ruto ambaye hakuungana na viongozi wengine wa Afrika katika hafla ya kuapishwa kwa rais mteule wa Nigeria, Bola Tinubu jana.

Ilibainishwa kuwa Lavrov alifanya mkutano na uongozi wa Bunge la Kenya mjini Nairobi na kwamba awali kiongozi huyo alikutana na spika wa bunge la kitaifa nchini humo Moses Wetangula afisini mwake.

Lavrov amekuwa akifanya ziara katika mataifa ya Afrika katika siku za hivi karibuni, matukio ambayo wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kuwa huenda ni njia moja ya Russia kutafuta mbinu za kupata ushawishi barani Afrika. **RFI**

# AZAM YAIPIGIA HESABU YANGA FAINALI YA FA

**Na Saada Akida**

BENCHI la ufundi la klabu ya Azam limeanza kuupigia hesabu mchezo wao wa fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) dhidi ya Yanga kwa kupanga kuitumia michezo yao miwili ya ligi iliyobakia kama sehemu ya maandalizi kuelekea kwenye fainali hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kally Ongala, alisema kabla ya kucheza fainali hiyo wana michezo miwili ya kumalizia msimu na yote wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kukusanya alama zote sita kabla ya kuigeukia Yanga kwenye mchezo wa fainali.

**Azam FC watacheza mechi hizo mbili za mwisho kwenye ligi ambapo Juni 3 watakuwa ugenini kucheza na Coastal Union kabla ya kurejea Dar es Salaam kuumana na Polisi Tanzania Juni 9.**

Alisema michezo hiyo miwili itakuwa mwanzo wao wa maandalizi kuelekea kwenye mchezo wa fainali kombe la FA ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Tunatambua umuhimu wa kila mechi zilizopo mbele yetu tunafanya maandalizi mazuri kupata pointi pia mechi hizi mbili za kumaliza msimu itakuwa mwanzo wetu wa kujiandaa na mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho, tumeanza kuipigia hesabu mechi yetu ya fainali," alisema Ongala.

Aliongeza wanaandaa timu kwa ajili ya kumaliza vizuri Ligi Kuu kwa kukusanya pointi zote sita lakini kuiandaa timu kwa ajili ya mchezo wa fainali dhidi ya Yanga.

"Msimu huu haukuwa mzuri sana kwenye ligi, tumekosa ubingwa hivyo kombe pekee ambalo tupo kwenye mstari wa kuwania ni ili la Shirikisho, tunajipanga kuhakikisha tunafanikiwa kulipata ili tusitoke kapa msimu huu," alisema Ongala.

Alisema wanafanyia kazi udhaifu wao waliouona kwenye michezo iliyopita ili kuhakikisha wanakuwa kwenye kiwango kizuri kwenye mechi zilizopo mbele yao.



Mchezaji wa timu ya Soka ya Wanawake ya Bulls, Rahma Abdallah (kushoto), akimiliki mpira mbele ya mchezaji wa timu ya International All Stars kwenye mashindano ya soka ya 'Dar Youth Cup' kwa wachezaji chini ya miaka 15 yanayofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mashujaa FC mguu mmoja Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kufungwa mabao 4-1 juzi na Pamba FC kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, timu ya Mashujaa FC imefanikiwa kuvuka kigingi cha kwanza kuelekea kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Mashujaa FC ilicheza mchezo huo wa mtoano 'Play Off' dhidi ya Pamba na kufanikiwa kusonga mbele kwa jumla ya mabao 5-4 baada ya mchezo wa kwanza kuibuka na ushindi mnono wa mabao 4-0.

Mchezo wa juzi ulikuwa mchezo wa 'play off' ya mkondo wa pili ambapo wageni walihitaji sare au kufungwa si zaidi ya mabao 4-0 ili kufuzu hatua inayofuata.

Kwa matokeo hayo, Mashujaa sasa inamsubiri mshindi atakayepatikana kwenye mchezo wa 'Play Off' za timu kutokana Ligi Kuu zitakazoshika nafasi ya 13 na 14.

Mpaka sasa zikiwa zimesalia mechi mbili kabla ya Ligi Kuu kumalizika, timu zilizo kwenye hatari ya kucheza mchezo huo wa Play Off ni KMC inayoshika nafasi ya 13 na Mtibwa Sugar inayoshika nafasi ya 14.

Mashujaa FC inaisaka nafasi hiyo ili kuwafanya mashabiki wa Mkoa wa Kigoma kuwa na nafasi ya kuiona michezo ya ligi kuu ikichezwa mkoani humo tangu mara ya mwisho kutokea hivyo miaka 30 iliyopita.

Timu ya mwisho kutoka Kigoma kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa Mbanga FC ambayo ilishuka daraja katikati ya 1990.

Ilikuwa ni bahati mbaya kwa mabingwa wa Ligi ya Muungano mwaka 1990, Pamba FC, kwani kwa mara nyingine tena wamekosa nafasi ya kurejea tena kwenye Ligi Kuu, hivyo kusubiri bahati yao tena msimu ujao.

Msimu uliopita ilifanikiwa kuvuka hatua ya 'Play Off' ya ligi daraja la kwanza lakini ilikutana na upinzani mkubwa kutoka kwa timu kutoka Ligi Kuu, Coastal Union, ambapo kwenye mechi ya kwanza ya mchujo, ililazimishwa sare ya mabao 2-2 nyumbani Nyamagana, Julai 21, 2021, kabla ya kuadhibiwa kwa mabao 3-1 Julai 24, Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Tayari timu mbili kutoka Ligi daraja la kwanza zimepanda daraja na msimu ujao zitacheza Ligi Kuu, timu hizo ni JKT Tanzania na Kitayosce.

## Bingwa Ligi Kuu Zanzibar kujulikana Juni 4

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KITENDAWILI cha nani ataibuka bingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu uwenda kikateguliwa Juni 4 ambayo imetangazwa kuwa ndio siku ya mwisho ya msimu wa ligi hiyo.

Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar imetangaza Juni 4 kuwa ndio siku ya mwisho msimu huu ambapo timu zote zitakuwa uwanjani kucheza michezo yao ya mwisho.

Mpaka sasa kwa mujibu wa msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ, klabu ya KMKM inaongoza ligi ikiwa na pointi 66 ikiwa ni pointi moja tu zaidi ya wapinzani wao wa karibu timu ya KVZ (65).

Katika michezo hiyo ya mwisho, KMKM itavaana na Chipukizi kutoka Pemba wakati KVZ wenyewe wataumana na Dulla Boys ambayo tayari imeshashuka daraja.

Wakizungumza na gazeti hili makocha wa timu hizo kuelekea michezo hiyo itakayoenda kuamua ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar kila mmoja anaamini kuwa atafanya vizuri na kufanikiwa kutwaa taji hilo.

## Stumai Mchezaji Bora Ligi Wanawake Mei

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa JKT Queens, Stumai Abdallah, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Ligi ya Soka ya Wanawake kwa mwezi Mei.

Stumai alikuwa na mchango mkubwa katika mwezi huu na kuisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa ligi hiyo illiyomalizika hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Stumai amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi baada ya kupachika mabao yaliyoisaidia timu yake hiyo kutwaa ubingwa ikiizidi pointi moja tu Simba Queens waliokuwa mabingwa kwa misimu mitatu mfululizo.

Hadi ligi inamalizika, Stumai anakamata nafasi ya tatu kwa upachikaji mabao, ambapo mshambuliaji wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa, alitwaa kiatu cha dhahabu akimaliza na mabao 17, Donisia Minja wa JKT Queens akiwa na pili kwa mabao 15, huku Stumai akifungana na Winfrida Charles wa Alliance Girls wote wakiwa na mabao 13 kila mmoja.

Hata hivyo, pamoja na kutwaa uchezaji bora wa mwezi huu, mchezaji huyo hakuteuliwa kuingia kwenye kinyang'anyiro cha tuzo ya mchezaji bora wa mwaka itakayotolewa hivi karibuni na Kamati ya Tuzo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF).

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRUNO ATAKIWA BARCA

BARCELONA inataka kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes, lakini klabu hiyo inaamini itapaswa kutoa ada ya uhamisho ya takriban euro milioni 100 ili kuwashawishi Newcastle United kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Times)***

### FIRMINO AFIKIRIWA

REAL Madrid inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31, ambaye atakuwa mchezaji huru mkataba wake na Liverpool utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

### POCHETTINO MIAKA MITATU

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino mwenye umri wa miaka 51, ametia saini mkataba wa miaka mitatu kuwa kocha mkuu mpya wa Chelsea. ***(Guardian)***

### ANCELOTTI NA BRAZIL

BRAZIL bado ina matumaini ya kumshawishi kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti kuwa kocha wao mkuu ajaye. Mabingwa hao mara tano wa dunia wamekuwa bila kocha tangu Tite alipoondoka baada ya fainali za Kombe la Dunia huko Qatar Desemba. ***(Athletic)***

### SAVIC AWINDWA

LIVERPOOL inaweza kumsajili kiungo wa Lazio Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 28, kwa euro milioni 26, huku mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia ukitarajia kumalizika 2024. ***(Calciomercato via Goal)***

### MAN YATAKA NYOTA

MATUMAINI ya Manchester United kumsajili beki wa Korea Kusini, Kim Min-jae mwenye umri wa miaka 26 na mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye miaka 24 kutoka Napoli yameongezeka huku kukiwa na uvumi kuhusu mustakabali wa kocha wa timu hiyo ya Italia, Luciano Spalletti. ***(Givemesport)***

### NEWCASTLE NAO WAMTAKA

KLABU ya Newcastle United pia imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kutaka kumsajili Kim Min-jae wa Napoli. ***(Fijaches)***

### O'BRIEN AFUATILIWA

KLABU ya Sheffield United inamfuatilia kiungo wa kati wa Nottingham Forest, Lewis O'Brien mwenye umri wa miaka 24, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo DC United. (Sun)

### LERMA KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Bournemouth na Colombia, Jefferson Lerma mwenye umri wa miaka 28, kwa uhamisho huru msimu huu wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

### SANCHEZ AITAKA EPL

MSHAMBULIAJI wa Chile ambaye yupo huru, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 34 anatamani tena kurejea katika Ligi Kuu ya England - baada ya kuzichezea Arsenal na Manchester United wakati huu akimaliza mkataba wake Marseille. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFICHUA KUWA NA MAJERUHI KABLA YA FAINALI

**LONDON,** England

PEP Guardiola amekiri kuwa hajui kama Kevin De Bruyne na Jack Grealish watakuwa fiti kwa ajili ya fainali ya Kombe la FA wikiendi ijayo.

**Wachezaii hao wawili na beki Ruben Dias walikosa kwenye kichapo cha 1-0 katika siku ya mwisho dhidi ya Brentford kutokana na majeruhi.**

Mabingwa hao wa Ligi Kuu, ambao watamenyana na Manchester United kwenye uwanja wa Wembley Jumamosi wanajaribu kutaka kubeba mataji matatu kihistoria, walifungwa bao la dakika za lala salama la Ethan Pinnock.

Huku De Bruyne na Grealish wakikosekana na Erling Haaland akiachwa kwenye benchi, walichezeshwa Phil Foden na Riyad Mahrez.

> ●●● Nina uhakika tungekuwa na tabia tofauti kidogo ikiwa tungehitaji...

Lakini Guardiola alisema: "Hongera sana Brentford kwa ushindi huo. Ni ngumu kuwashtua, jinsi wanavyocheza haraka, jinsi walivyo wakali katika idara zote.

"Nina uhakika tungekuwa na tabia tofauti kidogo ikiwa tungehitaji alama.

"Sina malalamiko yoyote ya jinsi tulivyofanya. Niliwaambia wachezaji baada ya mchezo, 'Leo tumemaliza Ligi Kuu mlishinda vilivyo. Furahia siku mbili na familia zako, tuonane Jumatano tutajiandaa kwa fainali ya kwanza'.

"Vijana ambao hawakucheza, kawaida hucheza, walikuwa wamechoka jana (juzi) Walihitaji kupumzika ili kuwasili wakiwa na nguvu sahihi kukabiliana na United."

Alipoulizwa ikiwa wachezaji waliokosa watakuwa fiti Wembley, Guardiola alisema: "Sijui kwa sasa.

"Ruben, Jack na Kevin hawakuweza kucheza. Ndivyo ilivyo. Nadhani watakuwa tayari lakini ni ngumu kujiandaa katika mazoezi. Ndio maana nililazimika kuwaona wachezaji waliocheza leo (juzi)."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 598,
MECHI KALI
FENERBAHCE
VERSUS
ANTALYASPOR
1 | 1.41
X | 4.52
2 | 6.51
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MBAPPE MCHEZAJI BORA UFARANSA



**PARIS,** Ufaransa

MCHEZAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe alitawazwa kuwa mchezaji bora wa Ligi ya Ufaransa, Ligue 1, kwa mara ya nne mfululizo Jumapili.

Fowadi huyo wa Ufaransa ndiye mchezaji pekee aliyeshinda tuzo hiyo mara nne, akiipiku rekodi aliyokuwa nayo Zlatan Ibrahimovich.

"Nataka kuwashukuru wachezaji na wafanyakazi wote kwa kile kilichofanyika," alisema Mbappe mwenye umri wa miaka 24. "Siku zote nilitaka kuacha alama. Sikutarajia kushinda mapema kiasi hicho, lakini nina furaha kuweka historia katika nchi yangu."

Mbappe ana mkataba na PSG hadi 2024 huku kukiwa na kipengele cha kuuongeza mwaka mmoja zaidi.

"Nina furaha na nitakuwa hapa msimu ujao," alisema, bila kutoa kidokezo juu ya kama atakaa katika klabu hadi 2025.

PSG walishinda taji la Ligi wakiwa wamesalia na mchezo mmoja baada ya kutoka sare ya 1-1 na Strasbourg Jumamosi.

Franck Haise alichaguliwa kuwa kocha bora wa msimu baada ya kuiongoza Lens hadi nafasi ya pili, ambayo itashuhudia klabu hiyo ya kaskazini ikicheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza baada ya miaka 21.

"Ni hadithi ya misimu mitatu. Wale ambao hawako kwenye hatua hii tena, siwasahau," alisema Haise, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa klabu hiyo mwaka 2020.



# Willian ataka kubaki Fulham

**LONDON,** England

WILLIAN anataka kusalia Fulham, ingawa uamuzi bado haujafanywa kuhusu mustakabali wa Mbrazil huyo.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea na Arsenal mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Cottagers Septemba mwaka jana na amekuwa mchezaji muhimu msimu huu.

Vijana wa kocha Marco Silva walifungwa kwenye mechi ya mwisho ya Ligi Kuu 2-1 na Manchester United Jumapili, huku Willian akitengeneza bao la ufunguzi la Kenny Tete.

Hiyo iliwakilisha pasi ya tano ya Willian kwenye ligi msimu huu na mchango wake wa bao la 10 la moja kwa moja kwenye mashindano kwa Fulham.

Willian ambaye mkataba wake utamalizika hivi karibuni hana uhakika kama atasalia London lakini atafurahi kufanya hivyo.

Alisema: "Bado sijui, kusema kweli, sijui kitakachotokea. Wakati ujao ni wa Mungu.

"Nikikaa Fulham, hakika nitakuwa sawa, nitafurahi. Najisikia vizuri sana hapa ni klabu ambayo ilinipokea vizuri sana. Lakini ikiwa ni sehemu nyingine, nitajitahidi kufanya kadri niwezavyo.

"Bado sijaamua. Tutaona kitakachotokea wiki chache zijazo, ni nini nitaamua. Lakini kama ningeweza kusal
kwenye Ligi Kuu na Fulhar
litakuwa jambo zuri kwangu
Akifafanua kwanini alich
gua kurejea England akiv
na Fulham, Willian alisem
"Siku zote nimekuwa nil
ipenda Ligi Kuu. Hizo s
habari kwa mtu yeyote, ki
mtu anajua ni kiasi gani mir
ni shabiki wa ligi ya hapa.
"Ligi hii kwangu, ni ligi bo
zaidi duniani.
"Kuamua kwenda Fulha
ilikuwa ni muda wa wiki mo
hivi. Tayari nilikuwa Londor
"Nilikuja hapa ili kuwa ka
bu na hapa na kufanya m
zungumzo na meneja wang
Ilikuwa ni takriban wiki mo
kabla ya kuamua kwenda Fu
ham.

# MANULA APELEKWA AFRIKA KUSINI KWA MATIBABU

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba moja wa Simba, Aishi Manula ameondoka nchini jana kwenda Afrika Kusini kwa ajili ya matibabu baada ya kuumia hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa ya klabu hiyo, Manula ameondoka nchini akifuatana na daktari wa timu hiyo, Edwin Kagabo ambapo ataenda kusimamia matibabu ya golikipa huyo wa timu ya taifa.

Kagabo alisema Manula anaenda kwenye jiji la Johannesburg ambapo atafanyiwa upasuaji kutibu majeraha yake ya nyama za paja.

**"Matibabu yake yatahusisha upasuaji kwa hivyo kuhusu atakuwa nje kwa muda gani itategemea na upasuaji huo, baada ya upasuaji na ushauri wa madaktari wa huko ndipo tutajua Manula atakaa nje kwa kipindi gani," alisema Dk. Kagabo.**

Manula alipata majeraha hayo Aprili 7 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam wakati timu yake ikicheza mechi ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu na kumalizika kwa Simba kushinda mabao 4-1.

Baada ya mechi hiyo amekosekana kwenye mechi zote za Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la FA.

Kutokana na kukosekana kwake, kipa namba tatu wa timu hiyo, Ally Salim alichukua nafasi hiyo, akicheza kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu siku tatu baada ya mchezo wa ligi kuu kwenye Uwanja wa Highland Estates na Simba kufanikiwa kushinda bao 1-0.

Baada ya hapo Salim aliendelea kucheza akianza kwenye mechi zote mbili za nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya mabingwa watetezi, Wydad Athletic Club ya Morocco na michezo iliyofuata.

## ...Mayele anukia kiatu cha dhahabu

INATOKA UK. 24

"Huu ni msimu bora sana kwangu tangu nianze kucheza soka kwa sababu tangu nimeanza mpira, hasa kwenye michuano ya kimataifa sijawahi kufunga idadi hii ya mabao, huwa naishia matatu au mawili tu, inaonyesha ni msimu bora sana naomba niendelee hivi hadi mwisho wa msimu," alinukuliwa Mayele.

Mchezaji huyo alijiunga na Yanga akitokea AS Vita mwaka 2021, amepachika mabao saba mpaka sasa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kuanzia hatua ya makundi, lakini amepachika mabao 16 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na kuongoza kwenye orodha ya wafungaji.

Alianza kufunga mabao yake katika Kombe la Shirikisho dhidi ya Real Bamako kwenye mechi zote mbili nyumbani na ugenini, Februari 16 Yanga ikitoka sare ya bao 1-1 na akapachika bao moja kwenye mechi iliyochezwa Machi 8 jijini Dar es Salaam akiiongoza timu yake kushinda mabao 2-0.

Alifunga bao moja kwenye mechi ambayo Yanga iliifunga US Monastir ya Tunisia mabao 2-0 na akapachika mabao yote mawili dakika ya 74 na 81, akiipa ushindi wa mabao 2-0 timu hiyo dhidi ya Rivers United na Mei 17.




Mashabiki wa Yanga wakishangilia baada ya timu yao kupata bao la kusawazishi dhidi ya U.S.M Alger katika mechi ya fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho uliofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi, Yanga ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Nabi: Rekodi ugenini*

INATOKA UKURASA 24

ivu na kujituma mpaka kupata matokeo hayo.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kwa sababu tulifanikiwa kuwazuia wachezaji hatari wa Yanga, Azizi Ki na Musonda (Kennedy) lakini yule mshambuliaji wao Mayele licha ya kufunga bao zuri lakini kwa kiasi kikubwa wachezaji wangu hawakumpa nafasi ya kutuadhibu zaidi," alisema.

Alisema wanarudi Algeria wakiamini bado kazi haijaisha na wana kazi kubwa kwenye mechi ya marudiano kutokana na rekodi nzuri za wapinzani wao nje ya uwanja wao wa nyumbani kwenye michuano hiyo.

"Tutakaporudi nyumbani tunajiandaa kama tunaanza upya hiyo mechi kwa sababu nina imani Yanga watakuja kivingine tunatakiwa kujipanga vizuri kulingana na ubora wa wapinzani wetu wanapokuwa ugenini," alisema kocha huyo Benchikha.

Kwenye mechi ya marudiano itakayochezwa Jumamosi ijayo, Yanga inahitaji ushindi angalau wa mabao 2-0 kuweza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo namba mbili kwa ukubwa Afrika katika ngazi ya vilabu.



# 498,850

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/05/23 | 21:00 | Al Wehda vs AL Faiha | 2.61 | 3.51 | 2.49 |
| 02. 31/05/23 | 21:30 | Arab Contractors vs Ismaily SC | 2.31 | 2.86 | 3.31 |
| 03. 31/05/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Roma | 2.57 | 2.92 | 2.87 |
| 04. 01/06/23 | 01:00 | Fortaleza CE vs Palmeiras | 2.84 | 3.20 | 2.29 |
| 05. 01/06/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs NY Red Bulls | 2.71 | 3.13 | 2.62 |
| 06. 01/06/23 | 03:30 | Corinthians vs Atletico Mineiro | 2.90 | 3.11 | 2.30 |
| 07. 01/06/23 | 19:00 | Haras EL Hodood vs Aswan | 3.22 | 2.86 | 2.35 |
| 08. 01/06/23 | 20:00 | Jonkopings Sodra vs Osters IF | 2.87 | 3.50 | 2.29 |
| 09. 01/06/23 | 21:00 | Vestmannaeyjar vs HK Kopavogs | 2.69 | 3.21 | 2.40 |
| 10. 01/06/23 | 22:15 | Fylkir vs KR Reykjavik | 2.74 | 3.31 | 2.31 |
| 11. 02/06/23 | 02:00 | Sarmiento Junin vs NewellS Old Boys | 2.69 | 2.74 | 2.74 |
| 12. 02/06/23 | 20:30 | Austria Lustenau vs TSV Hartberg | 2.55 | 3.33 | 2.39 |
| 13. 02/06/23 | 20:30 | Josko Ried vs Wolfsberger AC | 2.47 | 3.28 | 2.49 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 30/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:30 | 4632 | Dalian Zhixing FC vs Dongguan Guanlian | 2.73 | 2.89 | 2.58 |
| 10:30 | 5579 | Zibo Qisheng vs Jinan Xingzhou | 5.79 | 3.72 | 1.52 |
| 12:00 | 2824 | Jihlava U19 vs Sigma Olomouc U19 | 2.81 | 3.85 | 2.07 |
| 13:00 | 1614 | QNK Quang Nam vs Huda Hue | 1.38 | 4.12 | 7.00 |
| 14:00 | 4206 | SQC Binh Dinh vs Hai Phong | 1.96 | 3.33 | 3.33 |
| 15:15 | 2721 | Cong Anh Nhan Dan vs K. Khanh Hoa | 1.39 | 4.31 | 6.37 |
| 15:30 | 3256 | Duzyurtspor vs Erzin Bld | 2.02 | 3.30 | 3.30 |
| 16:30 | 1476 | Stromsgodset 2 vs Brann 2 | 3.49 | 4.93 | 1.61 |
| 17:00 | 1761 | Valerenga IF 2 vs Aalesund 2 | 2.28 | 3.60 | 2.54 |
| 17:00 | 3582 | Ararat Yerevan vs Bkma Yerevan | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 18:00 | 1309 | Rigas Futbola Skola vs BFC Daugavpils | 1.11 | 7.25 | 16.58 |
| 18:00 | 1643 | MC Alger vs USM Khenchela | 1.46 | 3.53 | 7.48 |
| 20:00 | 1680 | Sarpsborg Sparta 2 vs Skeid Fotball 2 | 1.98 | 3.81 | 2.93 |
| 20:00 | 1704 | Zamalek vs Talaea El Gaish | 2.04 | 3.01 | 3.81 |
| 20:00 | 1822 | Stabaek Fotball 2 vs Grorud IL 2 | 1.63 | 4.41 | 3.70 |
| 20:00 | 3231 | Istanbulspor vs Adana Demirspor | 2.47 | 3.83 | 2.39 |
| 20:00 | 3735 | Start 2 vs Donn | 1.53 | 4.51 | 4.30 |
| 20:00 | 3766 | Sivasspor vs Konyaspor | 2.17 | 3.37 | 3.05 |
| 20:00 | 3892 | Fenerbahce vs Antalyaspor | 1.41 | 4.52 | 6.51 |
| 20:00 | 4446 | Randers vs Aarhus | 3.50 | 3.55 | 1.97 |
| 20:00 | 5010 | Giresunspor vs Trabzonspor | 2.51 | 3.46 | 2.52 |
| 20:00 | 5077 | Ankaragucu vs Galatasaray | 4.95 | 4.31 | 1.54 |
| 20:00 | 5587 | Fatih Karagumruk vs Kayserispor | 2.03 | 3.95 | 2.95 |
| 20:00 | 5793 | Alanyaspor vs Kasimpasa | 2.21 | 3.57 | 2.83 |
| 20:30 | 2672 | USA U20 vs New Zealand U20 | 1.26 | 4.76 | 10.15 |
| 21:00 | 4493 | VVV Venlo vs Almere City | 2.69 | 3.34 | 2.38 |
| 21:30 | 1460 | Sacachispas FC vs Colegiales | 2.64 | 2.80 | 2.75 |
| 21:30 | 4965 | CA Fenix vs Argentino De Quilmes | 2.23 | 2.81 | 3.38 |
| 21:30 | 5581 | Deportivo Laferrere vs Csyd Liniers | 2.18 | 2.90 | 3.36 |
| 21:45 | 2873 | Ballymacash Rangers vs Knockbreda | 2.01 | 3.76 | 2.89 |
| 21:30 | 5968 | Cagliari vs Parma | 2.05 | 3.24 | 3.40 |

### JUMATANO - 31/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1723 | Urawa Red Diamonds vs Sanfrecce Hiroshima | 2.88 | 3.09 | 2.28 |
| 18:00 | 2511 | MC Magra vs CR Belouizdad | 6.20 | 3.57 | 1.52 |
| 19:00 | 1298 | National Bank vs El Daklyeh | 1.94 | 3.06 | 4.11 |
| 20:00 | 5058 | Utsiktens BK vs Orebro SK | 2.20 | 3.36 | 3.15 |
| 20:00 | 5477 | Landskrona Bois vs Trelleborgs FF | 2.10 | 3.51 | 3.25 |
| 20:00 | 5752 | Eyupspor vs Bodrumspor | 1.90 | 3.33 | 3.54 |
| 20:00 | 5768 | Gefle IF vs GIF Sundsvall | 2.38 | 3.25 | 2.93 |
| 20:00 | 5891 | IK Brage vs Ostersunds | 2.28 | 3.36 | 2.99 |
| 20:30 | 1465 | Colombia U20 vs Slovakia U20 | 1.56 | 3.57 | 5.58 |
| 20:30 | 5742 | Brazil U20 vs Tunisia | 1.20 | 5.59 | 11.38 |
| 21:00 | 1354 | Al Nasr Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.32 | 5.35 | 8.13 |
| 21:00 | 1984 | AL Adalh vs Al-Ettifaq | 1.69 | 3.91 | 4.49 |
| 21:00 | 2175 | Dhamk vs Al Shabab Riyadh | 4.47 | 4.10 | 1.66 |
| 21:00 | 4610 | Al Khaleej Club vs Abha | 1.64 | 3.95 | 4.80 |
| 21:00 | 4776 | Al Ittihad Jeddah vs AL Tai | 1.31 | 5.35 | 8.56 |
| 21:00 | 4803 | Al Wehda vs AL Faiha | 2.66 | 3.42 | 2.49 |
| 21:00 | 5451 | Al Taawon vs AL Baten | 1.62 | 4.20 | 4.68 |
| 21:00 | 5953 | Al Hilal Riyadh vs Al Raed Club | 1.27 | 5.96 | 8.93 |
| 22:00 | 4363 | Sevilla FC vs Roma | 2.63 | 2.94 | 2.78 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Mei 30, 2023

Nipashe



Willian ataka kubaki Fulham

UKURASA 22



Mchezaji wa Yanga, Joyce Lomalisa (kulia), akimiliki mpira mbele ya mchezaji wa U.S.M Alger katika mchezo wa fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho uliofanyika juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. U.S.M iliibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi: Rekodi ugenini inanipa matumaini

## ●●● Asisitiza fainali haijaisha, wajipanga kupindua meza Algeria...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema rekodi ya kufanya vizuri ugenini inampa matumaini makubwa ya kwenda kupata matokeo mazuri katika mchezo wa pili wa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USM Alger nchini Algeria.

**Yanga juzi ilikubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye mchezo wa fainali ya kwanza uliofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kuhitaji ushindi usiopungua wa mabao 2-0 kuweza kutimiza ndoto ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo msimu huu.

Nabi alisema licha ya matokeo hayo mabaya nyumbani, bado wana matumaini ya kufanya vizuri kwenye mchezo wa marudiano na rekodi nzuri ya mechi za ugenini kwenye michuano hiyo, zinampa matumaini.

"Mpira wa sasa hivi ni wa matokeo popote, kufungwa nyumbani haimaanishi tayari tumeshindwa, tuna dakika 90 nyingine za kujiuliza, msimu huu tumecheza mechi nyingi nje ya Tanzania na zipo ambazo tumeonyesha ubora wetu na kupata matokeo chanya," alisema Nabi.

Alisema kutokana na aina ya mchezo waliocheza juzi bado hajakata tamaa na wana uwezo wa kwenda kupata matokeo mazuri ugenini.

Yanga katika michuano hiyo msimu huu, ilianza kwa kucheza na Club Africain ya Tunisia kuwania nafasi ya kutinga hatua ya makundi.

Katika mchezo huo Yanga ilianza kwa kutofungana kwenye mchezo uliochezwa Dar es Salaam na kwenda kuwashangaza 'Waarabu' hao nyumbani kwao baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 na kutinga hatua ya makundi.

Kwenye hatua ya makundi mabingwa hao wa Tanzania walipangwa na TP Mazembe, Real Bamaco na Monastir.

Yanga ilifanikiwa kushinda mechi zote mbili nyumbani na ugenini dhidi ya TP Mazembe, ilitoka sare ya bao 1-1 ugenini na Real Bamaco lakini ilipoteza ugenini kwa mabao 2-0 dhidi ya Monastir na kuibuka vinara wa kundi lao.

Hatua ya robo fainali Yanga ilipangiwa kucheza na Rivers United ya Nigeria ambapo iliibuka na ushindi wa ugenini wa mabao 2-0 kabla ya kutoka 0-0 kwenye mchezo wa marudiano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kusonga mbele kucheza hatua ya nusu fainali.

Nusu fainali Yanga ikiwa ugenini Afrika Kusini iliiduwaza Marumo Gallants kwa kuifunga mabao 2-1 na hivyo kutinga fainali kwa jumla ya ushindi wa mabao 4-1 kufuatia ushindi wa mabao 2-0 walioupata awali jijini Dar es Salaam.

Rekodi hiyo nzuri kwenye mechi za ugenini ndizo zinazompa matumaini makubwa Nabi ya kushinda mechi ya marudiano jijini Algers Jumamosi ijayo.

"Kinachotakiwa ugenini ni kutafuta matokeo na kucheza kwa kujituma hadi tone letu la mwisho la jasho, tumeweza kufanya hivi kwenye mechi zetu za nyuma tukiwa Congo, Mali, Tunisia na hata Afrika Kusini, bado tuna nafasi ya kufanya vizuri, mashabiki wa Yanga hawana haja ya kukata tamaa, tutaenda kupambana kwa ajili yao na kwa ajili ya nchi," alisema Nabi.

Alisema upungufu mdogo ulionekana kwenye mchezo wa juzi wanaufanyia kazi na anataka kuona wachezaji wake wanatumia kila aina ya nafasi watakayoipata kupachika mabao.

Kuhusu hali ya Stephen Aziz Ki ambaye alishindwa kuendelea na mchezo, Nabi alisema nyota huyo amepata shida kidogo sehemu ya mgongo na leo (jana) wanatarajia kupokea taarifa kutoka kwa daktari kuhusu hali yake.

Katika hatua nyingine, Kocha wa USM Alger, Abdelhak Benchikha, alisema kwake bado fainali haijaisha licha ya matokeo mazuri ya ugenini waliyoyapata.

Alisema mechi haikuwa rahisi kwa sababu ya hali ya hewa ya mvua lakini anawapongeza wachezaji wake kwa ustahimil-

INAENDELEA UKURASA 23

## ...Mayele anukia kutwaa kiatu cha dhahabu CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa juzi na mshambuliaji hatari wa Yanga, mkongomani Fiston Mayele katika mechi ya fainali ya kwanza ya kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USMA ya Algeria, limemfanya kufikisha idadi ya mabao saba na kuwa kinara kwenye orodha ya wafungaji bora wa michuano hiyo.

Kwa mujibu ya takwimu za Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, Mayele amepachika mabao saba, akifuatiwa na straika wa Marumo Gallants ya Afrika Kusini, Ranga Chivaviro ambaye ana mabao sita, lakini timu yake iikiwa imeshatolewa.

Mchezaji wa Asec Mimosas, Kouame Kramo amefunga mabao manne, pamoja na Khaled Bousseliou wa USM Alger na Paul Acquah wa Rivers United.

Zinneddine Belaid wa USM Alger amefunga mabao matatu kwenye michuano hiyo mpaka sasa pamoja na Mustapha Mohamed wa Pyramids ya Misri na wachezaji wengine wengi ambao timu zao zimeshatolewa.

Mayele anaweza kukosa ufungaji bora kama wachezaji wa USM Alger, Bousseliou na Belaid watafunga mabao zaidi ya manne kwenye mchezo wa marudiano hatua ya fainali Jumamosi ijayo dhidi ya Yanga.

Kwa kifupi Mayele tayari amejiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa tuzo ya mfungaji bora wa michuano hiyo na kuendeleza nyakati bora za kucheza soka kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa AS Vita ya nyumbani kwao Congo.

Mayele wiki iliyopita alinukuliwa akisema msimu huu ndio msimu bora zaidi tangu aanze kucheza soka kutokana na ubora alionao kwa kufunga mabao mengi muhimu yaliyoisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kufika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >